# KUCHUNGUZA USAWIRI WA MUHUSIKA MWANAMME KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: JOKA LA MDIMU NA WATOTO WA MAMA N'TILIE

**KHAMIS ISSA MOHAMMED**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2018**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma Tasnifu hii iitwayoKuchunguza **Usawiri wa Mwanamme katika Riwaya ya Kiswahili: *Joka La Mdimu na Watoto wa Mama Ntilie,*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi Jamii katika Isimu ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**....................................................**

**Dkt. Mohamed Omary Maguo**

**(Msimamizi)**

**Tarehe**.............................

## TAMKO

Mimi **Khamis Issa Mohammed,** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu halisi, na kwamba, haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya masharti ya kupata shahada yoyote.

Saini…………………………………….

Tarehe…………………………………….

## HAKI MILKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe kazi nzima au sehemu ya kazi hii bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, isipokuwa kwa shughuli halali, kama vile kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma.

## SHUKURANI

Kwanza, napenda kumshukuru Mwenye-enzi Mungu (SW) Muumba wa Mbingu na Ardhi muweza wa kila kitu, kwa kunijaalia afya njema, nguvu, uwezo, akili, busara, maarifa, utulivu na uvumilivu katika kipindi chote cha masomo yangu ya uzamili. Namshukuru tena kwa unyenyekevu pamoja na tauhidi kwa kusema, Alhamdulillah Rabbilaalamina. Pia sala nasalamu ziende kwa kipenzi chake.Pamoja na shukurani hizi niwashukuru pia wazazi wangu wawili Bwana Issa Mohammed Khamis na Bibi Bimkubwa Muhammad Khamis kwa kunizaa, kunilea na kunipeleka shule tokea maandalizi hadi kufikia leo hii naikamilishakazi hii. Mwenyezi Mungu awape kila la kheri.

Pili, napenda kumshukuru kwa dhati kabisa, msimamizi wangu Dkt. Mohamed Omary Maguo kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu. Hakusita wala hakuchoka kunishauri na kuirekebisha kazi hii katika hatua zote mpaka ilipokamilika. Amenilea kitaaluma na kunipa moyo pamoja na kunifunza misingi ya nadharia za fasihi, fasihi fafanuzi na mbinu za utafiti ambazo zimezaa kazi hii. Namuomba Mwenyezi Mungu ambariki na ampe afya njema pamoja na ukakamavu, amzidishie kila la kheri, na kumuepusha kila la shari, Amiin.

Tatu, napenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu waliouonyesha kwa kuelewa kuwa nilikuwa masomoni, kwani kwa baadhi ya nyakati walinikosa na waliukosa upendo wa baba. Nne, napenda kuwashukuru walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kunilea kitaaluma na kunikuza kinadharia na vitendo. Walimu hao

ni Profesa E. Mbogo, Profesa T.Y. Sengo, Profesa S. Mdee, Dkt. P. Lipembe, Dkt Mohamed Omary Maguo pamoja na Bwana Bakari Kombo Bakari.

Tano, napenda tena kumshukuru Mwenye-enzi Mungu, kunipa nguvu na uwezo wa kuniwezesha kuichapa kazi hii ya tasnifu na kuiwezesha kuiwasilisha kwa wakati muafaka.

Sita, ninatoa shukurani zangu za pekee kwa wake zangu vipenzi Habiba Abeid Twahir, Raya Rashid Sultan, Maryam Said Juma na Iptisam Hamad Abdalla kwa ushawishi, uvumilivu, huruma na kunitia moyo pale nilipokata tamaa katika masomo yangu. Pia kwa msaada wa hali na mali katika kukamilisha masomo yangu, ikiwa ni pamoja na gharama za masomo na kuwa wasimamizi na nguzo imara na thabiti katika kuhakikisha sikati tamaa ila ninamaliza masomo yangu, tangu shahada ya kwanza mpaka sasa shahada ya pili (Uzamili).

Saba, ninawashukuru pia wanangu wote kutoka tangu wakwanza wao Safaa Khamis Issa hadi wa mwisho wao kwa sasa Balqiis Khamis Issa, pia kaka zangu wote na dada zangu wote pamoja na wakwe zangu wote kwa uvumilivu wao katika kipindi chote cha masomo yangu. Ni matumaini yangu kuwa wataweza kutambua umuhimu wa elimu katika maisha ya mwanandamu ili iwe ni changamoto kwao.

Mwisho, Nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitomshukuru Mwalimu wangu Shekhe Khamis Salim Ali kwa mchango wake wa hali na mali ikiwa ni pamoja na kuniruhusu kujiunga na masomo haya na kunitakia dua ya mafanikio kwa muda wote nikiwa masomoni.

## TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa Mama yagu mpendwa Bibi, Bimkubwa Khamis Muhammad kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, kunifunza mema, kunikataza mabaya, na kunipa moyo na kuniwezesha kifikira na maadili mema katika kipindi chote cha masomo yangu, tangu maandalizi, darasa la kwanza, mpaka sasa ninapokamilisha masomo yangu ya shahada ya Uzamili. Mawazo yake na busara zake katika elimu nitazikumbuka daima na kuwa chachu ya kujiendeleza zaidi.

## IKISIRI

Mada ya utafiti huu ni Kuchunguza Usawiri wa mhusika mwanamme katika riwaya ya Kiswahili: Joka la Mdimu na Watoto wa Mama N'tiliye. Malengo mahususi yalikuwa mawili ambayo ni kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika mwanamme katika riwaya teule na kuelezea usawiri wa mhusika mwanamme kama unavyojitokeza katika riwaya teule. Sampuli ya utafiti huu ilikuwa ni riwaya mbili teule ambazo ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Data za utafiti zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usomaji makini na upitiaji wa nyaraka na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa mwanamme katika riwaya teule anakabiliwa na changamoto za umasikini, rushwa, ulevi wa pombe na wanawake na kukosa uaminifu. Hivyo, kwa mapana zaidi usawiri wa mwanamme unaojitokeza katika riwaya teule ni kuwa mwanamme anasawiriwa kama mtu asiyefikiri bila kupata kilevi, asiyekuwa mwaminifu, mtu mwenye uelewa wa mambo, mtu mwenye huruma, mpumbavu, anayependa ugomvi, aliyelaaniwa, mfanyakazi ngumu, mtetezi wa wanawake, mtu asiyechoka wala kuona aibu, mbakaji na mnyanyasaji, asiyejiamini, anayedanganyika haraka, mwenye mapenzi kwa watoto na mtu asiyependa familia yake. Kwa jumla, imebainika kuwa mwanamme kama ilivyokuwa kwa mwanamke naye pia ana mambo mazuri anayoyafanya na kumpamba lakini pia anayo mambo mabaya ambayo kwa kawaida hapaswi kuwa nayo lakini kwa sababu ni binadamu hawezi kuyakwepa ni lazima yampate au ayafanye.

# YALIYOMO


ITHIBATI .................................................... i

TAMKO .................................................... ii

HAKI MILKI .................................................... iii

SHUKURANI .................................................... iv

TABARUKU .................................................... vi

IKISIRI… .................................................... vii

YALIYOMO .................................................... viii

**SURA YA KWANZA : UTANGULIZI .................................................... 1**

1.0 Utangulizi .................................................... 1

1.1 Usuli wa Tatizo Ia Utafiti .................................................... 1

1.2 Tatizo la Utafiti .................................................... 4

1.3 Malengo ya Utafiti .................................................... 5

1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti .................................................... 5

1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti .................................................... 5

1.4 Maswali ya Utafiti .................................................... 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti .................................................... 5

1.6 Mipaka ya Utafiti .................................................... 6

1.7 Mpangilio wa Utafiti .................................................... 7

**SURA YA PILI : MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .................................................... 8**

2.0 Utangulizi .................................................... 8

2.1 Dhana ya Riwaya .................................................... 8

2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Usawiri wa Mwanamke........................................... 9
2.3 Pengo la Maarifa........................................................................................... 17
2.4 Mkabala wa Nadharia .................................................................................. 18
2.4.1 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ................................................................ 18
2.4.2 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ............................................................ 22
2.5 Hitimishi ...................................................................................................... 23

**SURA YA TATU : MBINU ZA UTAFITI.............................................................. 25**

3.0 Utangulizi .................................................................................................... 25
3.1 Umbo la Utafiti............................................................................................. 25
3.2 Data za Utafiti Zilizokusanywa ................................................................... 26
3.2.1 Data za Msingi.............................................................................................. 26
3.2.2 Data za Upili................................................................................................. 27
3.3 Mbinu za Kukusanya Data .......................................................................... 27
3.3.1 Upitiaji wa Nyaraka...................................................................................... 27
3.3.2 Usomaji Makini ............................................................................................ 28
3.4 Sampuli na Usampulishaji ........................................................................... 29
3.5 Uchambuzi wa Data za Utafiti ..................................................................... 30
3.6 Hitimishi ...................................................................................................... 30

**SURA YA NNE : UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTAFITI .................................................................... 31**

4.0 Utangulizi .................................................................................................... 31
4.1 Kubaini Changamoto zinazomkabili Mwanamme ....................................... 31
4.1.1 Changamoto ya Umasikini ........................................................................... 32

4.1.2 Changamoto ya Rushwa ... 35
4.1.3 Changamoto ya Ulevi ... 38
4.1.3.1 Changamoto ya Ulevi wa Pombe ... 38
4.1.3.2 Changamoto ya Ulevi dhidi ya Wanawake ... 39
4.1.4 Changamoto ya Kukosa Uaminifu ... 40
4.2 Usawiri wa Mwanamme katika Riwaya Teule ... 41
4.2.1 Usawiri wa Mwanamme kama mtu asiyeweza kufikiri bila ya Kilevi ... 43
4.2.2 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu asiye Muaminifu ... 44
4.2.3 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Muwelewa ... 46
4.2.4 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu mwenye Huruma ... 47
4.2.5 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Mpumbavu ... 47
4.2.6 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu anayependa Ugomvi ... 49
4.2.7 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu aliyelaaniwa ... 50
4.2.8 Usawiri wa Mwanamme kama *Mtu wa kufanya kazi Ngumu* ... 51
4.2.9 Usawiri wa Mwanamme kama Muombezi na Mtetezi wa Wanawake ... 52
4.2.10 Usawiri wa Mwanamme kama mtu Asiyechoka wala kuona Aibu ... 53
4.2.11 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Mbakaji na Mnyanyasaji ... 54
4.2.12 Mwanamme amesawiriwa kama Mtu Asiejiamini ... 54
4.2.13 Usawiri wa Mwanamme kama mtu Asiyejitambua ... 56
4.2.14 Mwanamme ni Mtu anayedanganyika Haraka ... 56
4.2.15 Mwanamme ni Mtu mwenye Mapenzi Makubwa kwa Watoto wake ... 57
4.2.16 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu asiyependa Familia yake ... 59
4.3 Hitimishi ... 60

**SURA YA TANO: MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ....... 62**

5.0 Utangulizi .......... 62

5.1 Muhutasari .......... 62

5.1.1 Dhumuni Mahususi la Kwanza .......... 63

5.1.2 Dhumuni Mahususi la Pili .......... 63

5.2 Hitimishi .......... 64

5.3 Mapendekezo ya Utafiti .......... 64

5.3.1 Mapendekezo ya Kitaaluma .......... 65

5.3.2 Mapendekezo ya Kijamii .......... 65

5.3.3 Mapendekezo kwa Watafiti wa Usoni .......... 65

**MAREJELEO….. .......... 66**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.0 Utangulizi

Mada tunayoichunguza inahusu usawiri wa mwanamme katika dhamira za riwaya mbiliteule; *Joka La MdimuNa Watoto Wa Mama Ntilie ambazo zimeandikwa na Abdalla J. Safar na Emmanuel Mbogo.* Utafiti huu umejengwa sura tano. Sura ya kwanza, imeelezea mambo ya msingi kuhusu mada ya utafiti. Mambo hayo ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, vikwazo vya utafitina namna ya vikwazo hivyo vitakavyotatuliwa. Sura ya pili ilielezea kazi zilizosomwa na mtafiti, zinazohusiana na mada husikailikayotafitiwa. Pia, sura hiyo ilielezea nadharia zilikazomuongoza katika utafiti huo. Sura ya tatu imebainisha mbinu zilizotumika kukusanyia data na kuzichambua. Mbinu hizo ni pamoja na mbinu ya usomaji makini, ambayo ilitumika kuzisoma kwa makini kazi teule. Aidha data za utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Sura ya nne imeshughulikia uchambuzi wa data zilizokusanywa na mtafiti. Sura ya tano ilieleza matokeo ya utafiti, ambapo sura ilitathimini madhumuni mahususi ya utafiti huu na kumalizia kwa kutoa mapendekezo.

## 1.1 Usuli wa Tatizo Ia Utafiti

Wataalamu mbali mbali wameelezea na kufafanua maana ya riwaya. Kutokana na ukweli huo ni dhahiri kuwa kuna maoni mbali mbali yanayohusu dhana ya riwaya, maneno ambayo yamekaririwa na watalamu wote, ni kuwa riwaya ni utanzu wa fasihi andishi, kama ulivyo ushairi na tamthiliya. Matteru (1976) anafafanua kuwa riwaya ni hadithi ndefu ambazo zimeandikwa. Kutokana na maana hii tunaweza

kuona mambo matatu makuu katika dhana ya riwaya, kwamba riwaya ni hadithi, hadithi ni lazima iwe ndefu na ni lazima iwe imeandikwa.

Mphalele (1976), anasema riwaya ni hadithi ndefu za maneno kati ya 35,000 na 50,000. Tunaweza kusema kwamba kuna riwaya ndefu na riwaya fupi, kulingana na idadi ya maneno yaliyotumiwa na mwandishi. Mulokozi (1996) anaeleza kuwa, riwaya ni kazi ambayo inakuwa na sifa mbali mbali, kuwepo na ubunifu, usimulizi (ni hadithi ya kisimulizi la kinathari), mpangilio au msuko fulani wa matukio (ploti), mfungamano wa wakati, visa vinatendeka katika wakati fulani, inatakiwa iwe na maneno mengi na itakapokuwa na maneno pungufu ya elfu tatu (3000), yaweza kuitwa Novela, pawepo na mawanda mapana (kwa upande wa yale yanayozungumzwa, wakati na mahali pa matukio hayo), na pia pawepo na uchangamani katika visa, dhamira, tabia, wahusika n.k.

Senkoro (1982) na Wamitila (2002) wanaeleza kuwa riwaya ni kisa mchangamano ambacho huweza kuchambuliwa na kupimwa kwa mapana na marefu kifani na kimaudhui. Kisa ambacho urefu unaoruhusu kisa kitambe na kutambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwanadamu. Hivyo riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii.

Kuhusiana na chimbuko au chanzo cha utanzu huu wa fasihi, wataalamu wengi au wote wanakubaliana na chanzo cha riwaya ni hali halisi ya kijamii, pia wanakubaliana kuwa utanzu huu ni mchanga, ukilinganisha na tanzu kama ushairi, michezo ya kuigiza au tamthiliya.

Ndungo na Wafula (1991) wanasema kuwa, miongoni mwa riwaya za mwanzo kuzuka ilikuwa ni riwaya ya *Robinson Cruisoe* (1719) ya Daniel Defoe. Riwaya hii ilizuka kutokana na maendeleo na mabadiliko ya uvumbuzi wa viwanda. Ukoloni na uvumbuzi wa viwanda ulileta haja ya kueleza mambo kwa njia ya hadithi na ngano ambazo zilikuwepo kwa wakati huo. Wanaendelea kusisitiza kuwa, kuzuka kwa miji na viwanda kulistawisha uandikaji wa riwaya na usomaji kupanuka. Maendeleo katika vipengele vyote vya maisha kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii, yalizusha haja ya kuwa na utanzu wa fasihi ambao uchangamano wake wa kifani na kimaudhui ungedhibiti nyanja hizi zote.

Suala la kuchunguza nafasi ya mwanamme katika riwaya ya Kiswahili ni geni kwani hakuna mtafiti hata mmoja ambaye ambaye ameshughulikia. Hii haina maana kuwa utanzu wa riwaya ya Kiswahili haujafanyiwa utafiti la hasha. Wapo wataalamu kadhaa ambao wametafiti riwaya za Kiswahili kwa malengo mbalimbali. Njogu na Chimerah (1999) wamegusia riwaya kadhaa katika uhakiki wao na kubainisha kuwa riwaya ya Kiswahili imepiga hatua kubwa sana ya maendeleo katika karne ya 21 ikilinganishwa na karne zilizopita. Maelezo haya ni sahihi na tunakubaliana nayo kwa sababu ni katika karne ya 21 ndipo viwanda vingi vya uchapaji vilianzishwa na hivyo kutoa fursa kubwa ya kuchapwa kwa vitabu vya riwaya. Naye Chuachua (2011) alichunguza Itikadi katika riwaya za Shaaban Robert na kubaini masuala mbalimbali ya kiitikadi kama vile mapinduzi, umoja na mshikamano, upendo, imani ya dini, kuheshimu imani au dini za wengine nakadhalika. Maelezo haya ni muhimu katika kusukuma mbele utafiti wetu kwa msingi kwamba kupitia itikadi unaweza pia kupata usawiri wa mwanamme na hata mwanamke katika kazi za fasihi. Kwa jumla,

kazi za riwaya za Shaaban Robert zimetoa nafasi kubwa sana kwa mwanamme kushiriki katika masuala ya umma ikiwa ni pamoja na uongozi kuliko mwanamke.

Kwa upande wake Ambrose (2014) aliangalia masuala ya kisiasa katika riwaya za Shaaban Robert za Kusadikika na Kufirika na kubainisha kwamba, riwaya hizi mbili ni za ukombozi ambapo wananchi walikuwa wanataka uhuri wao kutoka kwa wakoloni. Hata hivyo, ni wanamme ndio wanaonekana kuwa na nafasi kubwa katika harakati za ukombozi licha ya kuwa mtafiti hakuonyesha hivyo na ni kwa sababu halikuwa katika malengo yake kufanya hivyo. Hivyo, tumeamua kufanya utafiti huu wenye lengo la kuchunguza usawiri wa mhusika mwanamme katika riwaya za *Joka la Mdimu* iliyoandikwa na Safari Jumbe na *Watoto wa Mama N'tiliye* iliyoandikwa na Emmanuel Mbogo ili kukuza maarifa zaidi katika eneo la usawiri wa wahusika wanamme katika riwaya ya Kiswahili na fasihi kwa jumla.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Katika ulimwengu wa riwaya ya Kiswahili na fasihi kwa jumla imekuwa ni jambo la kawaida kuona watafiti wengi wakivutiwa kuchunguza nafasi ya mwanamke zaidi kuliko nafasi ya mwanamme (Mulokozi, 1989; 1996 na 2002). Jambo hili limetokana na ukweli kuwa wanawake wamekuwa wakipiganiwa haki zao ili kuwafanya wawe sawa na wanamme katika nyanja za elimu, uongozi, ajira, kumiliki mali nakadhalika (Ndungo na Wafula, 1993; Ramadhani, 2013; Kengeru, 2013). Hii ni njia nzuri ya kumkomboa mwanamke kutokana na hali ngumu ya maisha inayomkabili kutokana na mfumo dume uliokithiri katika jamii (Senkoro, 1976; Mung'eri, 2000; Ntarangwi, 2004). Hali hii imefanya ukweli uliokuwa wazi ukasahaulika, nao ukweli huo si mwingine bali ni nafasi ya mwanamme katika riwaya za Kiswahili. Baada ya kuliona

hili ndipo sasa tukaamua kufanya utafiti wa kuchunguza nafasi ya mwanamme katika riwaya za Joka la Mdimu na Watoto wa Mama Ntiliye.

### 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una lengo kuu moja na madhumuni mahususi matatu yafuatayo:

#### 1.3.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza usawiri mhusika mwanamme ndani *Joka La Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie*

#### 1.3.2 Malengo Mahususi ya Utafiti

(i) Kubainisha changamoto zinazomkabili mhusika mwanaume kama zinavyojitokeza katika riwaya teule.

(ii) Kuelezea usawiri wa mhusika mwanamme kama unavyojitokeza katika Riwaya teule.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

(i) Ni changamoto zipi zinaomkabili mhusika mwanamme katika riwaya teule?

(ii) Mhusika mwanamme anasawiriwa vipi katika riwaya teule?

### 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu mkubwa wa kitamaduni, kitaaluma, kinadharia na kimuelekeo. Kwa uapande wa Kitaaluma utafiti huu utawasaidia wahadhiri, walimu na wanafunzi pamoja na watafiti kwa kuangalia usawiri wa mwanamme katika kazi nyengine za kifasihi ili waendeleze utafiti zaidi wa taswira ya mwanamme katika fasihi kupitia riwaya au tamthilia au kazi nyengine zozote za kifasihi.

Kinadharian utafiti huu huenda ukaibua mjadala unaohusiana na nadharia juu ya taswira ya mwanamme, hasa kwa wale wenye mtazamo pweke wanaona hakuna haja ya kuangazia taswira ya mwanamme kwakuwa mwanamme nikiumbe kisicho na kasoro na wala hakihitaji mtetezi.

Kiutamaduni utafiti umekuwa ni kama chanzo cha kujengautamaduni wa kuelewa kwamba, mwanamme na mwanamke ni jinsia mbili muhimu sana zinazosawiriwa katika riwaya ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Waandishi wengi huzitumia jinsia mbili hizi kama wahusika katika riwaya zao. Hivyo, ili tuweze kutatua matatizo yaliyomo katika jamii zetu nilazima tujenge utamduni wa kumuangalia mwanamke na mwanamme jinsi waandishi walivyowasawiri ndani ya kazi zao, hasa katika karne hizi za leo.

## 1.6 Mipaka ya Utafiti

Emanuel Mbongo anazo riwaya kama vile *Siri ya Maisha*, *Vipuli vya Figo* nah ii ya *Watoto wa Mama'tilie*. Lakini riwaya yake ya *Watoto wa Maman'tilie* na ile ya Safari ya *Joka la Mdimu* ndizo zinazohusika na mada ya utafiti huu. Vitabu vyengine vya Mbogo havitohusika. Maeneo yanayoangaziwa kwenye vitabun teule zaidi ni yale yaliyohusu maudhui kwenye kipengele cha dhamira. Vipengele vya fani havitoangaziwa kwenye uchambuzi wa utafiti huu. Pia mtafiti atajishughulisha na vitabu ambavyo vimeandikwa na waandishi wengine ikibidi ili kutoa ithibati au mifano ya ziada**.**

## 1.7 Mpangilio wa Utafiti

Utafiti huu umeundwa katika sura tano ambapo sura ya kwanza imetoa utangulizi juu ya usuli wa utafiti, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali na umuhimu wa utafiti. Sura ya pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi na machapisho mbalimbali yaliyopitiwa katika kazi hii, ikiandamana na mkabala wa kinadharia iliyomuongoza mtafiti kufanya kazi hii, ambapo mtafiti alitumia nadharia tatu katika kukamilisha kazi hii na kuifanya ionekane na maana. Sura ya tatu emeeleza mbinu za utafiti, eneo la utafiti, njia za kukusanya data na njia za uteuzi wa walengwa. Wakati sura ya nne inahusu uwasilishaji, uchambuzi wa mjadala kuhusu usawiri wa mwanamme kupitia vitabu teule, sura ya tano imetoa muhtasari, matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.0 Utangulizi

Sura hii imefanya kazi ya kupitia kazi tangulizi mbalimbali ambazo zinahusiana na mada ya utafiti ili kuona watafiti watangulizi wanazungumzia nini kuhusiana na mada ya utafiti wetu. Tumeanza kwa kuelezea kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti.

## 2.1 Dhana ya Riwaya

Waandishi waliobobea katika suala la riwaya kama Matteru na Muhando (1976) waliwahi kusema kuwa riwaya ni kazi ya kubuni kama hadithi ambayo hutungwa na kuibua mambo mengi katika mazingira wanayoishi watu. Naye Nkwera (1990) anasema kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kutungwa kwa kubuniwa iliyojengwa kwa tukio la kihistoria kueleza maisha ya watu au taifa fulani.Riwaya kwa kawaida huwa na muhusika mkuu mmoja au hata wawili. Senkoro (1982) anasema kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye wahusika zaidi ya mmoja yenye kueleza maisha ya watu.Riwaya ni kazi ya fasihi andishi ambayo huwa ndefu na aghalabu riwaya moja hujaza kitabu kizima.Riwaya huwa nawahusika wengi na huangazia mawazo kadhaa. Aidha, riwaya hufanyika katika mazingira mbalimbali na aghalabu huchukua muda mrefu kulinganisha na hadithi fupi.

Maana hizi juu ya dhana ya riwaya zilizotolewa na wataalamu hawa tunakubaliana nazo kwa msingi kuwa riwaya ni kazi au hadithi ya kubuni ambayo inaakisi uhalisia wa maisha katika jamii kutokana na ukweli kuwa yale yaliyobuniwa yanatokana na

mazingira halisi ya jamii. Riwaya haitoi dhamira zake hewani bali huzitoa kutoka katika jamii kutokana na shughuli zao za kila siku. Pia, riwaya ni lazima iwe na wahusika ambao ndio hutumiwa na mtunzi katika kubeba dhamira ambazo hadhira inatakiwa izipate.

## 2.2 Kazi Tangulizi Kuhusu Usawiri wa Mwanamke

Kama tulivyokwishatangulia kusema hapo awali, kazi tangulizi ambazo mtafiti amelazimika kuzirejele katika ukusanyaji wa data za utafiti huu ni usawiri wa mwanamke na kuhamishia mawazo hayo kwenye kazi yakeinayohusu usawiri wa mwanamme katika dhima za riwaya za *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Hii nikutokana na kukosa kazi tangulizi za moja kwa moja zilizochunguza usawiri wa mwanamme. Imani ya mtafiti ni kwamba, kazi hizi zitatoa msaada mkubwa kwake katika kuthibitisha kuwa usawiri wa mhusika wa kike ndio uliochukua nafasi kubwa katika fasihi ya Kiswahili ikilinganishwa na usawiri wa nafasi ya mwanamme katika fasihi na hususani riwaya ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Beauvoir (1949), utiifu hauhusishwi miongoni mwa majukumu ya mwanamke. Alidai kuwa, kila mwanamke nchini Ufaransa ana uhuru wa kujiamulia mambo lakini nyanjani uhuru huo haupo. Ni uhuru kidhahania kwa sababu hauambatani na uhuru wa kiuchumi. Mwanamke anayemtegemea mumewe hawezi kuwa na uhuru wa kujiamulia mambo kwa sababu mila na desturi hazimruhusu. Hali kama hii ni yakini katika baadhi ya mataifa na jamii hususan bara la Afrika. Uhuru ambao ni hasi haujaleta mabadiliko kwa mwanamke. Amekubaliana na hali yake ya kuwa mwanamke huku akiishi kwa kuvumilia matatizo mengi. Ni kupitia kwa ajira ambapo mwanamke ataweza kujinasua kutokana hali na ya unyanyasaji unaotokana

na mila.Hakuna njia nyingine mwafaka ambayo inaweza kumhakikishia uhuru wake maishani isipokuwa hiyo ya ajira. Pindi tu atakapoacha kuwa mtegemezi na kujitosheleza katika baadhi ya mahitaji, mfumo wa kutegemewa utabadilika na hatakumbana na madhila mengi yanayohitaji kuangaziwa au mtu wa kutegemea kuleta suluhu la masaibu yanayomkumba duniani. Kule kumtegemea mwanamume ndiko huyu mwanaharakati anadai kuwa ni chanzo cha unyonyaji. Jamii haijaweka mikakati ya kutosha ili kuleta mabadiliko kuhusu hali ya wanawake kutumishwa. Kazi hii ya Beauvoir ni muhimu kwa mtafiti wa kazi hii, kwa sababu imetaja unyanyasaji unaotokana na mfumo wa kijamii. Lakini bado unyanyasaji huu haubaki kwa wanawake tu, wako na wanaume wanaonyanyasika katika jamii zao au taasisi zao wanazofanyia kazi. Si hayo tu, pia katika karne hizi za Sayansi na Teknolojia wako wanaume wengi ambao hawana maamuzi ndani ya majumba yao, maamuzi yote yako chini ya wake zao au wazee wao wa kike. Unyanyasaji  ni kipengele miongoni mwa vipengele alivyovichunguza mtafiti kama changamoto zinazosababishwa na baadhi ya wanajamii hususani wanawake. Sasa ulimwengu huu una baadhi ya sehemu ambazo zinathibitiwa na mifumo ya kijamii ambayo huwakweza wanawake na kuwatweza wanaume. Mpaka sasa hakuna kundi la wanaume ambao wana imani inayofungamana na misingi ya kisiasa ambao wamechukua hatua ya kujiunga na kuunda vyama vinavyowasaidia kutetea haki zao tu kama uchunguzi wetu ulivyodhihirisha katika kazi hii.

Haya yote yanaleta mvuto wa kufanya uchunguzi kuhusu hali ya wanamme hasa kuhusu taswira.

yao kulingana na waandishi mbalimbali. Kazi hii pia ilikuwa ni muhimu kwa mtafiti wa kazi hii kwa sababu ilimsaidia mtafitikuangalia namna mwanamme alivyosawiriwa na Safari katika kitabu chake cha *Joka LaMdimu* na Mbogo katika kitabu chake cha *Watoto Wa Mama Ntilie*.

Mukobwa (1985) ameshughulikia "Maendeleo ya kimaudhui katika tamthilia za Ebrahim Hussein." Amezungumzia kipengele cha maudhui ambacho vile vile mtafiti wa kazi hii amekishughulikia huku akiangazia usawiri wa mwanamme. Mukobwa (keshatajwa) alitumia nadharia ya ki-Marx kujikita katika uhalisi wa kihistoria, lakini mtafiti wa kazi hiiametumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ili kumuongozakuangazia taswira ya mwanamme. Mtafiti wa kazi hii anakubalianana ufafanuzi wake kuhusu taswira ila yeye amekusanya data yautafiti wake kutoka tamthilia za Hussein, mwandishi wa jinsia ya kiume na mtafiti wa kazi hiiamekusanya dataza utafiti wake kutoka katika riwaya mbili tofauti za Safari kwa upande mmoja na Mbogo kwa upande wa pili wakiwa wote ni waandishi wa riwaya tena wajinsia ya kiume. Kipengele cha maudhui kilimsaidia mtafiti wa kazi hiikuyachunguza mawazo ya Safari na Mbogo kutokana na usawiri wao wa mwanamme ndani ya vitabu vyao viwili tulivyoviteua.

Chesaina (1987) alitumia tamthilia ya Mlama (1972) *'Hatia'* na tamthilia ya Muhando (1982)

'*Nguzo mama'* na kueleza utata unaomkabili mwanamke katika hali zake zote za maisha. Tofauti na yeye ni kwamba mtafiti wa kazi hiialitumia *Joka La Mdimu na Watoo Wa Mama Ntilie* ambapo anahisi kwamba kazi yake ni yenye msaada katika

kuangazia masaibu yanayomkumba mwanammehasa kwakuyachunguza waliyoyaandika kuhusu *Joka La Mdimu na Watoto Wa Mama Ntilie*. Utata anaouzungumzia Mhando (keshatajwa) ulikuwa kwa mtafiti wa kazi hii ni darubini yakuangazia taswira ya mwanamme katika kazi yake.

Katola (2006) ameshughulikia "*Udhalimu dhidi ya wahusika wa kike katika tamthilia nne za Kiswahili."* Tamthilia hizo ni za waandishi wa jinsia tofauti ambao ni Muhando, *Hatia* (1972), Mwachofi *Mama Ee* (1987). Hawa ni waandishi wa kike. Waandishi wa kiume ni Yahya na Mulwa, *Buriani* (1983) na Mohamed *Kitumbua kimeingia mchanga,* (2000). Katika kazi yake hakuegemea upande wowote wa waandishi ila ameonyesha kuwa mwanamke anadhulumiwa na mifumo ya kiume katika taasisi ambazo zimejikita kwenye misingi ya ubabe-dume. Baadhi ya dhuluma alizozibainisha ni pamojana wanawake kutishwa, kutusiwa, kuozwa bila hiari, kupigwa, kunyimwa haki na kukataliwa na jamii miongoni mwa zingine. Matokeo yake ni mtazamo hasi kwa mwanamke katika jamii. Katola (keshatajwa) ametumia nadharia ya ufeministi waKiafrika. Kazi hii imekuwa ya manufaa sana kwa mtafiti wa kazi hiikwa sababu mtazamo wake kuhusu dhuluma ulimpatiamwanga mtafiti kutambua zile dhuluma kama changamoto ambazo zinaweza kutafutiwa suluhu mwafaka na kupunguzwa kwa sababu haziwezi kukomeshwa kabisa.Pia kwa kuipitia kazi ya Katola (keshatajwa) mtafiti ameonadhulma wanazofanyiwa wanawake jinsi zinavyohamishiwa kwa wanaume nabado wahakiki na wataalamu mbalimbali wanaendelea kukaa kimnya tu.

Kazi ya mtafiti wa kazi hii inatofautiana na kazi ya Katola (keshatajwa) kwa sababu mtafiti wa kazi hii ametumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ambayo misingi yake

imo kwenye mahusiano ya umma, kazi za sanaa na miundo ya jamii. Mwelekeo wa mtafiti wa kazi hii utasaidia kugundua ikiwa madai mengine nyeti kama vile 'haki' na 'usawa'yanakubalika kulingana na kaida za kijamii au ni kwa jinsi gani mfumo wa kisheria utasaidia kuinua kiwango cha utekelezwaji. Pia mtafitin wa kazi hiiatajaribu kuchunguza sehemu ambazo dhana ya 'usawa'haiwezi kuwa na uhalisia. Dhana ya usawa kukosekana ni yakinifu kulingana na Honore de Balzac (1799-1850) jinsi alivyonukuliwa na Coser (1963) kuwa: *"Usawa ni 'haki' lakini hakuna mamlaka wala nguvu hapa duniani ambayoyanaweza/zinaweza kugeuza dhana hii kuwa ya kweli na halisi".*

Lugano (1989) aliandika na kuonyesha picha ya mwanamke katika siasa na mambo ya kijamii kwa kumulika riwaya za Kezilahabi. Alionyesha kuwa mwanamke anachorwa kama kiumbe anayetegemea mwanaume. Kauli hii ni kwa mtafiti wa kazi hii kwa sababu itamsaidia kuchunguza nakubainisha uhalisia wake na athari zinazoibuka kutokana na taswira hii. Mirengo ya nadharia zote za kijamii humulika mifumo ya jamii na katika mfumo wowote ule, kipengele cha utegemezi hakiwezi kukosekana. Kipengele hiki kitamsaidia mtafiti wa kazi hii kuchunguza taswira ya mwanamme kwa kujikita katika riwaya za wandishi tuliowateuwa.

Mwita (2005) anasema kuwa, kutokana na mfumo wa kuumeni uliokithiri katika jamii ya Wakuria, hali halisi ya mwanamke inaonekana iliyojaa dhulma, unyanyasaji na unyonyaji. Mwanamke daima ni mtegemezi. Hali zote za maisha yake hutegemea uamuzi wa mwanamume. Kujiamulia mambo kwa wanawake katika jamii hiyo ni sifa hasi. Anatamatisha kwa kusema kuwa hali hii ni yakini katika jamii nyingi za Kiafrika. Tatizo linalojitokeza hapa Mwita (keshatajwa) aliangalia jamii ya Kikuria

tu amesahau kudarumini jamii nyengine za Kitanzani hasa za mijini ambapo unyanyasaji wa wanamme umekithiri.

Mtafiti wa kazi hii kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi anakubliana na mawazo ya Mwita ila kipindi tulicho nacho kwa sasa hali imebadilika. Kipindi cha miaka yanyuma hali ilikuwa jinsi Mwita anavyoeleza. Mabadiliko tunayoyashuhudia sasa yameletwa na maendeleo ya elimu ya mtoto msichana na uhamasishaji unaoendelezwa na wanaharakati wakisaidiana na baadhi ya wafuasi wa madhehebu ya kikristo. Pia mashirika yasiyo ya kiserikali yametoa na yanaendelea kutoa mchango kuhusu uhamasishaji wa umma juu ya maswala yanayowahusu wanawake. Kazi hii ni muhimu kwa mtafiti wa kazi hii kwa sababu imeweza kumsaidiakatika uchambuzi na uhakiki wa kazi za Safari  na Mbogo huku tukiangazia usawiri wa mwanamme. Hatahivyo kazi ya Mwita (keshatajwa) ni tofauti na kazi ya mtafiti wa kazi hii kwa kuwa uchunguzi Mwita (keshatajwa)ni kuhusu *"dhima ya ichingero za Wakuria katika kusawiri taswira ya mwanamke"*na uchunguzi wa kazi hiini kuhusu "*usawiri wamwanamme katika dhamira za Riwaya ya Joka La Mdimu na Watoto wa Mama Ntilie*". Uchunguzi wake ulikuwa wa uwandanina ule wa kazi hiiumetumia matini za riwaya.

Matundura Enock (2007) katika tasnifu yake kuhusu "*Taswira dumifu za uana katika fasihi ya Kiswahili ya watoto,*" kama anavyonukuliwa na Nguta (2011) anasema kuwa mkabala wa kiuana unajishughulisha na maswala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano yanajibainisha katika misingi mbalimbali kama vile kijinsia, kitamaduni, kiutendi kazi, kiu-asasi. Pia ametumia mkabala wa nadharia ya ufeministi ambao ni mkusanyiko wa 'nadharia' nyingi ambao kimsingi lengo lake ni kuleta usawa kati ya

wanawake na wanaume. Kazi hii imekuwa ya manufaa kwetu kwa sababu tumepata mambo muhimu ambayo tunafikiri yatajitokeza katika kazi yetu ili kuangazia usawiri wa mwanamme. Vipengele hivyo vimetusaidia kuchunguza mwelekeo ambao Profesa Safari na Profesa Emmanuel Mbogo kwa kupitia nadhariya ya Sosholojia ya Fasihi na nadharia ya Saikolojia Changanuzi wameegemea na kuibua taswira mbalimbali za mwanamme. Matundura pia amefafanua dhana za uana na jinsia. Amesema kuwa 'jinsia' ni dhana ya kibayolojia na 'uana' ni dhana ya kitamaduni. Dhana hizi mbili zitatusaidia kuangazia usawiri wa mwanamme kwa misingi hiyo. Ugavi wa majukumu hufanywa kuegemea dhana hizi mbili. Hata hivyo kazi yake ni tofauti na yetu kwa sababu amechunguza taswira dumifu za uana katika *Msichana mlemavu na ndugu zake, Mwanasesere wa Mosi* na*Mgomba changaraweni*. Pia ameangazia taswira dumifu katika *Ndoto ya Riziki, Siku ya wajinga*na *Alitoroka kwao.*

Kitali (2011) ameshughulikia fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* na *Mama Ee*. Kuhusu tamthilia ya *Pango,* anasema kuwa, tatizo kuu linahusu siasa, uchumi, uongozi na migongano ya wimbi la ukale na usasa. Kuhusu tamthilia ya *Mama ee,* anasema ni mchezo unaoyasawiri matatizo yanayoikumba ndoa ya Mwavita na mumewe Kinaya. Pia ameangazia mahusiano ya wanawake na wanaume katika jamii, nafasi ya mwanamke katika jamii, taasubi ya kiume na ubabedume ambao umejikita katika jamii. Sisi tutashughulikia taswiraya mwanamme katika riwaya mbili ambazo ni *Joka La Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie.* Tutajaribu kuchunguza jinsi mwandishi Profesa Safari na Profesa Mbogo walivyowasawiri wahusikawakuu kama mashujaa wa kupigania haki zao bila

kufanikiwa. Hata hivyo kazi za waandishi hawazitaendelea kuchunguzwa kama kichocheo cha wanaharakati wa kupigania haki za wanaume jambo ambalo limepuuzwa na waandishi wengi.

Mirikau (2011) alishughulikia *taswira ya mwanamke katika tamthilia za Wamitila*. Katika kazi hiyo, Mirikau amejitahidi sana kufafanua istilahi "taswira" kwamba, ni jinsi mtu anavyochorwa na kuweza kutoa picha kamili ya namna anavyoonekana. Anaendelea kueleza kuwa picha hii aghalabu hutokana na namna anavyofikiriwa kupitia mambo yanayopitikia akilini mwa binadamu. Mambo haya huweza kudhihirika kupitia matendo halisi anayotendewa. Mwanamke anatendewa na hata mwenyewe huweza kujitendea mambo ya kushangaza katika jamii husika. Anatamatisha kwa kusema kuwa, taswira hii ni kuhusu ngazi katika jamii ambayo mwanamke hujikuta amewekwa na kukubaliana na uamuzi huo unaomfanya aidha atukuzwe au adhalilishwe

na hata kujidhalilisha mwenyewe. Waandishi wa riwaya tulizoteua ni wa jinsia moja na kazi zao zina ukuruba mwingi. Mawazo ya Mirikau yametusaidia kuchunguza riwaya zetu teule ili kuyafikia malengo yetu kwa kumulika matendo anayotendewa mwanamme na kubainisha changamoto zinazomkabili katika mfumo wa kijamii.

Nguta (2011) ameangazia *fani na usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Pango na Mama Ee*. Kazi yake ni muhimu kwetu kwa kuwa yeye ameangazia 'fani' na vipengele vyake vyote. Sisi pia tutajikita katika riwaya ya *Joka La Mdimu* kwa upande mmoja na *Watoto Wa Mama Nilie* kwa upande mwingine, tofauti na Nguta. Waandishi wa tamthilia alizoteua ni wa jinsia tofauti ilhali tuliowateua ni wa jinsia

moja (kiume). Nguta ametumia nadharia mbili ambazo ni urasimu (ufani)na ile ya ufeministi. Sisi tutatumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi, Mwitiko wa Msomaji na Saikolojia changanuzi .Kwa mukhutasari,kazi ya Nguta imeangazia baadhi ya vipengele tunavyodhamiria kuangazia hivyo basi imetunufaisha kwa njia moja au nyingine hasa pale wahusika wameangaziwa jinsi wanavyotumia lugha katika mazungumzo baina yao na uzungumzi nafsia (balagha).

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wamezungumzia juu ya 'jinsia' na 'uana' katika kitabu chao *Isimu Jamii* kama vigezo vinavyotumiwa na jamii kuleta ubaguzi. Dhana ya 'uana' ni kigezo cha maumbile ambapo kibayolojia inadhihirisha kama mtu anayezungumziwa alizaliwa mke au mume na hali hii haibadiliki kamwe. Kwa upande mwingine uana ni dhana ya kisosholijia ambayo imezalika kutokana na nadharia ya ufeministi inayodai kuwa kijamii mwanamke na mwanamume wanayo majukumu tofauti tofauti. Suala la dhana ya uana ni tata mno kwa kuwa ni suala lililo na misingi ya kijamii au kisosholojia. Kwa mfano, mtoto anapozaliwa hupewa jina na hilo jina litatambulisha jinsia yake.

## 2.3 Pengo la Maarifa

Kimsingi, kati ya watafiti wote hawa tuliopitia kazi zao hakuna hata mmoja ambaye amechunguza nafasi ya mwanamme katika kazi ya fasihi. Wote wamemakinikia nafasi ya mwanamke tu jambo ambalo linaashiria kuwa ipo haja ya kushughulikia usawiri wa nafasi ya mwanamke katika riwaya za Kiswahili na ndio maana tukaamua kuchunguza usawiri wa nafasi ya mwanamke katika riwaya za *Watoto wa Mama N'tiliye* na *Joka la Mdimu* ili kuziba pengo la maarifa.

## 2.4 Mkabala wa Nadharia

Nadharia ni wazo kuu, fikira kuu, muongozo mkuu wa mtu au watu (jamii) wa pahala fulani wakati fulani kwa sababu fulani (Sengo, 1975). Kwa mujibu wa Senkoro (1982) nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomuelekeza msomaji wa kazi ya fasihi kuielewa kazi hiyo ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Mushengezi (2003) amesema kwamba nadharia ni maarifa yaliyopangwa ilikuelezea dhamira fulani au wazo fulani.

Nadharia huchukuliwa kuwa ni dira ya kumuongoza mtafiti au mchambuzi kulikabili na kulielezea vyema jambo fulani kwa mtazamo ambao mtafiti ameujengea imani kwamba unaweza kuleta manufaa zaidi kuliko mtazamo mwingine pindi ukitumika. Ni mawazo, maelezo au mwongozo uliopangwa ili kusaidia kutafuta au kuelekeza jambo fulani.

### 2.4.1 Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi

Mtafiti aliishughulikia kazi hii hukuakiongozwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi iliyoasisiwa na Georg Lukacs. Lukacs alirithi mawazo ya maendeleo ya kijamii na migongano ya kitabakakutoka kwa Karl Marx. Kwa mujibu wa Coser (1963) Sosholojia ya Fasihi ni kitengo maalumu cha uchunguzi ambacho humulika mahusiano baina ya kazi ya sanaa, umma na muundo wa kijamii na jinsi kazi hiyo ilivyojitokezana kutathminiwa ubora na uhafifu wake. Hunuia kueleza sababu ambazo zimechangia kuibuka kwa kazi ya sanaa iliyo na umbo lakijamii na jinsi fikra za ubunifu wa mwandishi zinavyoongozwana mila, desturi na mpangilio wa jamiihusika. (Hii ni tafsiri ni ya mtafiti mwenyewe). Kulingana na Coser (1963), binadamu ndiye kiumbe pekee aliye na uwezo wa kutumia lugha.

Kwa miaka mingi iliyopita, binadamu amekuwa akijishughulisha na ukusanyaji wa maarifa pamoja na kanuni za mwenendo maishani. Haya yote yameweza kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Anatamatisha kauli hii kwa kusema kwamba ni jamii za kibinadamu pekee zilizo na uwezo wa kuwa na mila. Tylor kama alivyonukuliwa na Coser (1963) kuhusu Sosholojia ya Fashi alitoa mchango kuhusu dhana ya utamaduni na akasema kwamba, ni dhana isiyoweza kuelezwa kwaurahisi kwa sababu ni changamano. Inahusu imani, mila, desturi, itikadi, maadili, sheria, elimupamoja na mazoea ambayo mtu huwa nayo kama mmoja wa wanajamii. Vipengele hivi nimuhimu kwa mtafiti wa kazi hiikwa sababu vilimsaidia mtafiti kuangazia usawiri wa mwanamme katika riwaya za*Joka La Mdimu na Watoto Wa Mama Ntilie.* Jamii zote zinazojulikana zimewaweka wanajamii katika matabaka kihadhi. Kuna tabaka la juu, kati na chini. Mchakato huu unahusu ugavi wa majukumu ya kila mtu kiumri, kijinsia na kihadhi huku utofauti ukibainika wazi kupitia umiliki wa mali, mamlaka na ukuu. Tofauti kati ya tabaka la juuna la chini, matajiri na maskini, watawala na watawaliwa, wenye nguvu na wanyonge ni vigezo vinavyotumiwa kuainisha makundi haya. Jinsi wanajamii katika makundi haya wanavyochukuliwa na kuhudumiwa, wanavyogawiwa majukumu na ukosefu wa haki sawa hubainisha mfumo wa kijamii. Sosholojia ya Fasihi pia huangazia mamlaka na nguvu kama mihimili ya kijamii. Kwa mujibuwa Coser (1963), mamlaka ni uwezo wa kuamua mwenendo au tabia ya watu wengine kulinganana matarajio ya mwenye mamlaka. Hakuna mahusiano ya kijamii ambapo elementi ya mamlakaitakosekana kabisa; hivyo basi kuna fikra kwamba dhana ya mamlaka ni msingi katika dhanazote za kisosholojia. Kwa kifupi, mamlaka ni zile nguvu ambazo mtu hupewa kulingana na kaidazinazokubalika na watu wawili au zaidi na kati ya makundi mawili au zaidi

kwenye mahusiano. Coser (1963) anamnukuu Max Weber aliyeainisha mamlaka na kuyaweka katika makundimatatu ambayo ni mamlaka ya kisheria, mamlaka ya mila na desturi (mapokeo) na mamlaka yakihaiba (charismatic).

Narizvi (1982) aliandika kuwa: uhusiano baina ya fasihi na jamii umekuwa mada ya mvuto katika uchunguzi wote wa kibinadamu.Wahakiki wa kazi zilizoandikwa na wanasosholojia wamekuwa wakijadili mada hii kutokana na mitazamo mbalimbali na kutoa kauli mbalimbali zenye ukweli kinzani kiasi cha kumkanganya mtu aliye na tajriba katika nyanja mahususi. Kulingana na Wellek na Warren (1954), uhusiano baina ya fasihi na jamii hujadiliwa kwa kutanguliza ufungamano wa fasihi na jamii. Wahakiki wa dhana hii wanadai kuwa ni makosa kuchukua fasihi kama kigezo cha kuashiria jinsi jamii yoyote ile ilivyo. Walidai kuwa kazi kama zile za mwandishi maarufu Shakespeare na tenzi za Milton au kazi ya Burke haziwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha jamii zao. Jinsi mwandishi anavyowasilisha kazi yake hutegemea tajriba, uzoefu na mtazamo wake kuhusu maisha hivyo basi itakuwa si kweli kufikiri kuwa kazi ya mtu binafsi ni kiashiria cha maisha ya jamii kwa ujumla katika jamii anamotoka. Mtazamo wa fasihi kupitia sosholojia, hutufanya tumchukue mwandishi kama zao la nguvu za kisosholojia za wakati wake na kuepuka kumpunguzia sifa za ubunifu asilia. Kulingana na James Sutherland (1957), "jinsi ambavyo mwandishi alivyoandika hutegemea kipindi alichoandika, tabaka ambamo alizaliwa, elimu aliyopokea pamoja na dini yake".

Pingamizi nyingine kuhusu matumizi ya elimujamii ya fasihi ni mtazamo wa mwandishi na nguvu za kisosholojia ambazo huchunguza sehemu teule na hivyo kuufanya mtazamo wa kijumla kukosa maana. Wahakiki wanashikilia dhana

kwamba uchunguzi wa fasihi unahitaji tuwe na wazo kuhusu kile ambacho ni muhimu na kile ambacho si muhimu. Wahakiki wanaopinga mbinu ya kisosholojia hawapingi kuwepo uhusiano baina ya fasihi upande mmoja na hali ya kijamii, uchumi na siasa upande mwingine.Uchunguzi wa kijamii kuhusu kazi ya maandishi au mwandishi mwenyewe utatusaidiakumchunguza mwandishi kama mwanachama wa jamii, athari za kijamii zilizomwathiri nakumpatia msukumo wa kubuni kazi ya sanaa. Kwa mfano sisi tutachunguza kazi za Profesa Safari na Profesa Mbogo ambazo ni za kisanaa.Sosholojia ya Fasihi inamzingatia binadamu kama uti wamgongo wa ulimwengu huu na sanaa kwa ujumla wake. Ndio maana mtafiti wa kazi hiiakaichagua nadharia ya Sosholojia ya Fasihi kumpatia msingi kuzichambua na kuzichanganua riwaya ya *Joka La Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie* kwa kuegemea mihimili yake.Kulingana na Mbuthia (2005), juhudi kubwa zimefanywa ili kupata uelewa zaidi kuzihusujamiikupitia uchunguzi wa kina wa kazi ambazo zimeaandikwa.Jambo hili linawezekanatu ikiwa mtafitiatachagua nadharia inayofaa. Kazi za Wellek na Warren (1963) zinabainisha uwezo wa Sosholojia ya Fasihi kuchanganua maswala haya. Nadharia ya Sosholojia ya Fasihi ilimfaa mtafiti kwakazi hii aliyoishughulikia. Kwa mujibu wa Wellek na Warren (1963:94); Kama nadharia yoyote ile, Sosholojia ya Fasihi ina wale wanaoipinga. Wapinzani wake wanadai kwamba, nadharia hii haisaidii kuchunguza uhusiano baina ya fasihi na mambo **y**akijamii, kiuchumi na kisiasa kwa sababu uhusiano hauwezi kujitokeza wazi katika kitengo chochote kile na hivyo basi umuhimu wake hauwezi kutathminiwa. Kwa mfano, katika kazi fulani, mada hujikita kwenye maswala ya kisiasa, kijamii, au mahusiano ya kiuchumi. Huu ni ukweli ingawa Sosholojia ya Fasihi haiwezi kugusia suala la umuundo au maumbo.

### 2.4.2 Nadharia ya Saikolojia Changanuzi

Nadharia ya Saikolojia Changanuzi, ni nadharia inayoangalia kazi ya fasihi na kuihusisha na mwandishi.Nadharia hii inaangalia kila alichokiandika mwandishi huwa kinatokana nafikira zake mwenyewe.Makero yake au jamii yake ambayo yamehifadhiwa katika ungamuzibwete na kutolewa katika njia ya Ndoto, Mizaha (Utani). Nadharia ya saikolojia changanuzi pia inazungumzia lugha ya ishara(yaani kila lugha au kitu alichokitumia mwandishi katika kazi yake huwa kinaashiria).

Mwasisi wa mwanzo wa nadharia hii anaitwa Sigmand Freud (1896) ambae anasema kwamba kila mtu anasehemu inayoitwa ungamuzibwete binafsi. Katika nadharia hii anaaminiwa kwamba fikra hasi za binaadamu hubuniwa nakuhifadhiwa katika ungamuzibwete. Fikra hizo hutokana na mikatale (vizuizi) ya kijamii, mila, tamaduni na kisiasa. Mikatale ya aina hiyo huzuiya kutolewa katika mazingira halisi na hatimaye hutolewa katika ndoto au utani (mizaha) au kupitia uandishi na itokeapo huitwa mitelezo ya kauli.

Wright: Yeye anaiita Saikolojia Changanuzi ya Kirasimu. Huitazama kazi ya fasihi kama mawazo ya ndoto na pia huiona kazi ya fasihi kama viashiria vya mawazo ya mwandishi (kilaanalolisema huwa linaashiria hisia za mwandishi). Nadharia hii huitazama kazi ya fasihi na kumuhusisha na mwandishi kama hisia zake.

Msingi mkuu wa nadharia ya Saikolojia Changanuzi ni kuihusisha kazi ya fasihi na maisha ya mwandishi, historia au jamii yake.Hii ni kusema alichokiandika mwandishi kitakuwa kimemgusa mwandishi au jamii ya mwandishi, hivyo katika nadharia hii motifu huchukuliwa na kuhusishwa na mwandishi mwenyewe na hasa

mivutano iliyomkumba au kuiyona akiwa mdogo na jinsi inavyojitokeza katika kazi yake. Uchanganuzi wa wahusika hawa huyahusisha wanayoyachanganua na saikolojia ya mtunzi na hali hiyo huitwa Saikolojia ya Kiid.

Ferdinal De Saussure: Yeye anasisitiza kuwa kila kitu kilichoandikwa na mwandishi wa fasihi ni ishara-hivyo kutakuwa na kiashirii na kiashiriwa.

Lacan: Anasema visehemu vilivyobanwa katika ungamuzibwete kama matamanio na kumbikizi (kumbu kumbu) huwa ni viashirii navyo huunganishwa kitaashira na kutumwa ni muandishi, yanapotumwa hutolewa mojakwamoja kama ishara.

Freud: Anakubaliana na Lacan na kusisitiza kuwa ungamuzibwete hujidhihirisha kupitiamatumizi ya lugha, ndoto, mizaha na mitelezo ya kauli ya kiishara, sitiari na taashira. Na pia nadharia ya Saikolojia Changanuzi hushughulika na:

(i) Nadharia ya saikolojia Changanuzi huchunguza akili ya binaadamu
(ii) Linaloandikwa huwa ni hisia za mwandishi binafsi, jamii yake au watuwake wa karibu.
(iii) Athari za kimazingira, historia, kisiasa na maisha ya jamii ni msingi wa nadharia hii.
(iv) Lugha ndiyo msingi wakuchunguza fasihi (kila kitu ni ishara).
(v) Mawazo hutolewa katika ndoto, mzaha na mitelezo ya kauli.

## 2.5 Hitimishi

Katika sura hii tumepitia kazi tangulizi ambazo kwa namna moja au nyingine zimesaidia katika kujenga pengo la maarifa katika tasinifu hii. Kazi tangulizi

zinaonyesha kuwa nafasi ya mwanamke ndiyo iliyoshughulikiwa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na ile ya mwanamme na ndipo hapo tulipovutiwa kutaka kuona na mwanamme naye anasawiriwa vipi katika riwaya za Watoto wa *Mama N'tiliye* na *Joka la Mdimu*. Pia katika sura hii tumewasilisha nadharia mbili za Sosholojia ya Fasihi na Saikolojia Changanuzi ambazo ndizo zilizotumika katika kuchambua data za utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imehusu mbinu mbalimbali za utafiti zilizotumika katika kukusanya na kuchambua data za utafiti huu. Sura hii ina vipengele kadhaa. Vipengele hivyo ni pamija na umbo la utafiti, eneo la utafiti, na mbinu zilizotumika kukusanyia data. Vipengele vingine ni mbinu za uteuzi wa data, wateuliwa, mipaka ya utafiti na vifaa vilivyotumika katika kukusanyia data.

## 3.1 Umbo la Utafiti

Lytuu (2011) amenukuu Orodha (2003) akisema kwamba umbo la utafiti au usanifu wa utafiti ni mpangilio unaohusutaratibu zinazotumika kukusanya na kuchambua data kwa namna ambayo inaunganisha data zilizopatikana na malengo ya utafiti. Kothari (2004) anafafanua kuwa kipengele hiki kinaonesha taswira au picha kamili ya utafiti husika kwamba utafanyikaje, lini, wapi, kwa muda gani na kwakutumia mbinu zipi zinazosaidia kupatikana kwa data zenye mantiki zinazojibu maswali ya utafiti husika. Utafiti huu umetumia umbo la kimaelezo. Kothari (1990), amesema kuwa umbo la kimaelezo ni njia ya kukusanyia data na kuzifanyia uchambuzi kwa njia ya kimaelezo ambapo nambari huwa hazitumiki. Hivyo, data za utafiti huu zilikusanywa na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kuzichambuadata kwa njia ya maelezo kutegemea madhumuni mahususi ya utafiti huu.

Umbo la utafiti pia hujulikana kwa jina lingine kama usanifu wa utafiti yaani *Research design*. Usanifu wa utafiti ni mchoro au ramani inayoonesha namna utafiti

utakavyofanyika tangu katika kukusanya mpaka kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti (Kombo na Tromp, 2006). Katika utafiti huu tumetumia uchunguzi kifani ambapo tumeteua riwaya za *Joka La Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie* na kuchunguza usawiri wa mwanamme katika vitabu hivyo. Uchunguzi kifani ni aina ya usanifu wa utafiti ambapo mtafiti huteua eneo au kitu maalumu cha kutafitiwa ili kutimiza malengo fulani ya utafiti (Kitula, 2010). Uchunguzi kifani ni mbinu yenye faida nyingi kwa mtafiti kwani kupitia mbinu hii mtafiti hutumiamuda wake vizuri kwa kuwa tayari amekwishafahamu ni kitu gani anachoshughulikia. Hii humfanya asitumie muda mwingi kushughulikia mambo mengine yasiyomuhusu na kupoteza muda. Mbinu hii pia humsaidia mtafiti kupata data anazozihitaji kwa urahisi zaidi na tena data hizo huwa ni za uhakika.

## 3.2 Data za Utafiti Zilizokusanywa

Katika utafiti wowote ule wa kitaaluma huwa kunakuwa na data za aina mbili. Data hizo ni za msingi na upili. Katika utafiti huu mtafiti amekusanya data za msingi na data za upili ili kuweza kukamilisha madhumuni ya utafiti wake.

### 3.2.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine yeyote kwa lengo na matumizi kama yanayofanywa na mtafiti wa kwanza (Furlong, 2000). Kothari (2004) yeye anaeleza kuwa data za msingi nizile zilizokusanywa kwa mara ya kwanza.Data za msingi pia hujulikana kama data ghafi ambazo ndiyo kwanza zinaingia katika taaluma ya utafiti kwa mara ya kwanza tayari kwa ajili ya kuchambuliwa na kuchanganuliwa. Data hizo zikishachambuliwa na kuandikwa katika ripoti au tasinifu hubadilika jina na

kuwa ni data za upili. Katika utafiti huu, mtafiti amekusanya data za msingi katika riwaya za *Joka La Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*.

### 3.2.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zilikwishakusanywa na watafiti wengine kwa ajili ya kutimiza malengo ya utafiti wao na kuandikwa katika ripoti, makala, majarida, tovuti na vitabu, tayari kwa ajili ya kusomwa kama marejeleo katika maktaba mbali mbali (Bryaman, 2004). Maktaba alizozitumia mtafiti wa kazi hiini Maktaba Kuu ya Chake Chake, Maktaba ya Chuo Kikuu Huria tawi la Pemba,Chuo Kikuu Cha Dar-es- Salaam na kadhalika.Katika maktaba hizi mtafiti amezisoma kazi nanyaraka mbalimbali kama vile Makala, tasinifu, majarida pamoja na vitabu vilivyolingana na kuingiliana na mada ya utafiti pamoja na malengo ya utafiti.

## 3.3 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (1999) anaeleza kuwa dhana ya ukusanyaji wa data kuwa ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusudia ili kufanikisha lengo lake la utafiti. Utafiti huu ulikusanya data zake kwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka na usomaji makini wa riwaya teule. Mbinu ya upitiaji wa nyaraka ilitumika katika kukusanya data za upili na mbinu ya usomaji makini ilitumika katika kukusanya data za msingi.

### 3.3.1 Upitiaji wa Nyaraka

Neno "nyaraka" kama lilivyotumika katika utafiti huu linarejelea machapisho na maandiko mbali mbali yanayopatikana katika maktaba. Kimsingi, mbinu ya upitiaji wa nyaraka maktabani ni mbinu ya kukusanya data za upili kwa mtafiti kukusanya

machapisho yanayohusiana na mada yake ya utafiti na kuyasoma kwa uzingativu (Kothari, 1990). Data za upili pamoja na kutumika katika kushadidia hoja zitokanazo na data za msingi katika uchambuzi wa data lakini pia hutumika katika uandishi wa sura ya pili ya tasinifu inayohusika na "mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Data za upili katika utafiti huu zilikusanywa kutoka katika machapisho yanayopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Makavazi ya Taasisi za Taaluma ya Kiswahili (TATAKI), Maktaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kituo cha Pemba na Maktaba ya serikali Pemba mjini Chake Chake. Katika maktaba hizi mtafiti alisoma makala, ripoti, tasinifu, majarida, vitabu na maandishi pepe katika wavutina tovuti zilizohusiana na mada ya utafiti wake.

### 3.3.2 Usomaji Makini

Usomaji makini au wakati mwingine hujulikana kama usomaji wa kina ni mbinu ya kukusanya data za msingi kutoka kwa watafitiwa matini zilizoteuliwa katika utafiti husika (Kothari, 1990). Kupitia mbinu hii, mtafiti huteua matini maalumu na kuzisoma kwa kina huku akidondoa baadhi ya maneno, sentensi au aya ambazo ndizo huwa data za utafiti wake. Tunasema ni mbinu ya usomaji makini kwa sababu mtafiti husoma kazi hizo tena na tena mpaka pale anapojiridhisha kuwa sasa amepata data alizokuwa anazihitaji katika kukamilisha malengo ya utafiti wake.

Data za msingi katika utafiti huundizo zilizokusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini kutoka katika riwaya za *Joka La Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie*. Katika kufanikisha zoezi la ukusanyaji wa data, mtafiti aliandaa daftari maalumu ambalo aliligawanya katika sehemu kuu tatu na kila sehemu ikiwa na kichwa cha

habari kinachohusiana na madhumuni mahususi ya utafiti wake. Hii ilirahisisha zoezi la ukusanyaji wa data zilizotakikana katika utafiti huu.

### 3.4 Sampuli na Usampulishaji

Furlong (2000), anaelezea kwamba uteuzi wa watafitiwa ni kitendo cha kuchagua au kupata kikundi fulani ili kuwakilisha kundi lengwa. Hivyo, katika utafti huu mtafiti ametumia uteuzi lengwa. Kwa mujibu wa Babbie (1999) anaeleza kuwa uteuzi lengwa ni ule wa mtafiti kwenda moja kwa moja kwenye chanzo cha data alizozihitaji ili kupata data za utafiti wake. Mtafiti alizichagua kazi za *Joka la Mdimu*na *Watoto Wa Mama Ntilie*, kwa sababu mtafiti ndizo riwaya alizozichagua. Hivyo, mtafiti aliamini kuwa, kazi hizo zitatoa picha ya uhalisia wa kile kinachotafitiwa.

Vitabu hivi viwili viliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa kwa sababu aliamini kuwa vitabu vya *Joka la Mdimu*na *Watoto Wa Mama Ntilie*vingempatia data anazozihitaji. Babbie (1999) anaeleza kuwa usampulishaji lengwa ni mbinu ya uteuzi wa sampuli ya utafiti ambapo mtafiti huteua sampuli fulani ya watafitiwa wake akiamini kuwa sampuli hiyo ni sahihi na ndiyo itakayompa data sahihi za kuweza kutimiza maelengo ya utafiti wake. Hivyo, mtafiti aliteua vitabu vya *Joka la Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie*kuwa ndio watafitiwa wake. Sampuli lengwa ina manufaa makubwa kwa mtafiti kwani humwezesha kupata data za uhakika tena kwa muda mfupi. Hii ni kwa sababu mtafiti hatumii muda mwingi kwenda kufanya utafiti kwa kundi ambalo halihusiki bali huegemea kwa watafitiwa watokanao na sampuli lengwa tu.

### 3.5 Uchambuzi wa Data za Utafiti

Uchambuzi wa data ni kitendo muhimu sana katika kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanapatikana na hivyo utafiti mzima nao kukamilika. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mbinu ya mkabala wa kimaelezo kuchambua na kujadili data za utafiti na matokeo yake. Kothari (1990) anaeleza kuwa mkabala wa kimaelezo ni mbinu ya uchambuzi wa data ambapo mtafiti huzichambua data zake kwa kuzitolea maelezo yanayohusiana na madhumuni ya utafiti wake. Mbinu hii hutumika sana katika kuchambua data zinazohusiana na fasihi kwa sababu fasihi ni taaluma ya maneno aidha ya kuandikwa au kuzungumzwa. Hata hivyo, haina maana kuwa katika uwasilishaji na uchambuzi wa data za utafiti hatuwezi kutumia mbinu ya mahesabu-huweza kutumika pia ila kwa utafiti huu, mkabala wa kimaelezo ndiyo mbinu ya uchambuzi wa data iliyotumika katika kuchambulia data za utafiti.

### 3.6 Hitimishi

Sura hii ya tatu ya utafiti tunaweza kuiita kuwa ni sura ya ufundi na utaalamu kwani imeeleza mambo ambayo yana msingi sana katika kuwezesha ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti. Katika kuufanya utafiti huukukamilika na kuweza kuaminiwa kitaaluma mtafitiamekusanya data za msingi na data za upili kwa kutumia mbinu za upitiaji wa nyaraka na usomaji makini wa riwaya zilizoteuliwa mutawalia. Data za upili zimetumika katika kushadadia hoja zitokanazo na data za msingi ili kuimarisha uchambuzi na matokeo ya utafiti kwa jumla. Pamoja na hayo, katika sura hii pia mtafiti ameelezeawatafiti wake ni nani/nini.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kuchambua data zilizopatikana katika utafiti huu kuhusiana na mada iliyofanyiwa uchunguzi. Utafiti huu ulilenga kuchunguza usawiri wa mwanamme katika maudhui ya riwaya za Kiswahili kwa kutumia mifano ya riwaya za *Joka La Mdimu na riwayaya Watoto Wa Mama N'tilie*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza usawiri wa mwanamme na kuonesha jinsi taswira hiyo ilivyotumika katika kuibua dhamira za kazi hizo. Utafiti huu umebaini kuwa, riwaya zote mbili zimeandikwa na wasanii wenye jinsia mojo yaani jinsia ya kiume. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inahusu Changamoto zinazomkabili mwanamme zinavyochangia kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii yake au taasisi anayoisimamia. Sehemu ya pili inaelezea juu ya Dhamira zilizojitokeza ndani ya riwaya mbili hizi *Joka La Mdimu* na *Watoto Wa Mama Ntilie*. Sehemu ya tatu inafafanua namna wandishi hawa wawili walivyomsawiri mwanamme kama shujaa, mtetezi wa wanawake, mpenda starehe, mtu mnyonge anayestahiki kazi ngumu za sulubu, mwenye huruma kwa mke na watoto, mtu asiyejali familia yake nakadhalika. Na sehemu ya mwisho ya sehemu hii ni hitimishi.

## 4.1 Kubaini Changamoto zinazomkabili Mwanamme

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikusudia kutazama changamoto mbalimbali zinazomkabili mwanamme kama zinavyojitokeza katika riwaya teule. Kutokana na kufahamu changamoto hizo itakuwa ni rahisi kwetu kuona usawiri wa mwanamme katika riwaya teule.

### 4.1.1 Changamoto ya Umasikini

Umasikini ni hali ya kutokutimiza mahitaji ya lazima yanayomlazimu mtu katika maisha ya kila siku (Msokile, 1993; Matteru, 1976). Mfano wa mahitaji hayo ni kama vile chakula, malazi, mavazi, huduma za kiafya nakadhalika.Kwa kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi na nadharia ya Sosholojia ya fasihi, pamoja na nadharia ya Mwiitiko wa Msomaji mtafiti amechambua changamoto tofauti zilizodhihirishwa nawaandishi wote wawili ; Profesa Safari na Profesa Mbogo kupitia vitabu vyao vya riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama Ntilie.* Waandishi hawa wanaonesha kuwa miongoni mwa changamoto zinazomkabili mwanamme nazinazochangia kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii au taasisi wanazofanyia kazi ni umasikini. Wasanii hawa wamedhihirisha umasikini uliokithirikwa kutumia wahusika wao wakuu waliowachora na kuwaswawiri katika riwaya zao. Tukimuangazia Mbongo katika riwaya yake ya Mama Ntile, anaona suala la umasikini ni changamoto kubwa inayochangingia kutofaulu kwa mwanamme kupata maendeleo ndani ya jamii yake. Mtafiti wa kazi hii kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amegundua kuwa suala la umasikini ni suala ambalo limeongelewa kwa kiasi kikubwa kaika riwaya hii. Takriban wahusika wote ambao wanakumbana na suala hili la umasikini ni wanaumekazi zao ni zakijungujiko zenye malipo hafifu (mkia wambuzi). Malipo hayo haziwezi kuwapatia kipato cha kutosha kuyamudu maisha. Hivyo ndivyo wanaume wengi waishivyo ndani ya Tanzania yetu hii. Katika riwaya hii ya *Watoto wa Mama Ntilie,* mwandishi anaonesha jinsi kijana wawa kiume Doto na Kurwa watoto mapacha walioachwa na baba yao baada ya kufariki umasikini unavyowaendeshaputa. Tunaambiwa na mwandishi kwamba maisha katika familia hii yalikuwa hayawezi kwenda bila ya

Mama Ntilie kuuza ugali au wali katika genge la Urafiki (uk.14). Mwandishi katika kuibainisha hoja hii anasema :

Ilikuwa saa 2 :30 hivi asubuhi. Nyumba haikuwa na mtu ila Peter. Alikuwa kakaa nje kiambazani akiwaza, akiota jua, « Leo nitakwenda nijaribu. »Tatizo alililoliona Peter ni moja tu. Nalo ni mama yake. « Je, angekubali mpango wake ? ». Mtoto Peter aliwaza. Mionzi ya jua ilimuunguza usoni, akainama kidogo, kijiti mkononi, anachimbua ardhi. Mara sauti ilimwita, « Peter wee ! » Peter aliitika. Alimuona Zenabu kasimama nje ya chumba chake.

Aliinuka, akaenda.
'Shikamoo dada.'
'Marahaba. Vipi ?'
'A-aa !' alitingisha kichwa.

Zenabu aliiona ile midomo mikavu iliyokaukiana. Aliona uso ule uliomparama na machoyenye vitongo tongo bado. Aliona miguu ile pekupeku yenye ngozi ilyokatika ikiwa migumu kama ya mamba.

Maelezo haya ya msanii yanatuonesha wazi hali ya umasikini alionao Peter. Midomo mikavu iliyokaukina inashiria wazi kukosa chakula cha kujikimu na miguu iliyopasuka mithili ya mamba nacho nikielelezo tosha cha umasikini. Miguu hii imepasuka kwa kukosa kuvaa viatu na badala yake anatembea pekupeku. Na mwandishi amemtumia muhusika Peter kwa makusudi kuonesha jinsi wanaume nao wanavyoathiriwa na changamoto hii ya umasikini na kupelekea wanaume wengi kujingiza kaika tabia chafu ya wizi.

Tukiangazia kwa upande wa Safari ndani ya kitabu chake cha *Joka La Mdimu* naye anatuonesha kuwa umasikini nimiongoni mwa changamoto zinazowakabili wanaume na kuchangia kwa kiasi kikubwa kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia. Kwa kupitia wahusika wake wakuu Mfano, Tino alifanya kazi ya kusukuma rikwama, Jinja Maloni alifanya kazi ya kuchimba makaburi na kupakua vyoo. Ukichunguza utaona wote hawa niwahusika wenye jinsia ya kiume ndio aliowabebesha changamoto hii ya umasikini kama kiashishiria cha jinsi ya wanaume Waafrika (Tanzania) walivyokumbwa na changamoto hii ya umasikini. Kwa kupitia nadharia alizoziteuwa mtafiti katika utfiti huu Mwandishi anaona mwanamme nikiumbe kilichokabiliwa na changamoto ombazo zinahitaji nazo kufikiriwa na kuandaa mbinu mbadala ili kumuona mwanamme naye napatiwa maisha bora na aondokane na maisha yale yakijungujiko. Kazi ngumu kama vile uchimbaji wa kaburi, kazi ambayo mara nyingi wachimbaji walipenda kusaidiwa na wenzao, lakini kutokana na umasikini Jinja Maloni kazi hiyo aliamua kuifanya pekeyake Mwandishi anasimulia:

Walipoondoka, Jinja Maloni alitia fedha zake mfukoni, akalaza kipimo kwa makini na kupigilia mambo kama ramani yake. Alilima kwa muda sehemu hiyo, kisha akatupa jembe pembeni na kuanza kutumia sururu. Alichimba hivyo kwa robo saa, akatupa sururu chini. Udongo bado ulikuwa bado mbichi na pote nyasi zilikuwa zimestawi vizuri. Aliokota chepeu lake na kuanza kutupa udongo nje ya kaburi.

> Wachimba makaburi wengi walipenda kusaidiwa na wenzao. Na hakika zamani kazi hiyo ilifanywa na watani au ndugu wa karibu wa marehemu, hasa vijana bila ya ajira. Shughuli hiyo nzito ya simanzi haikuhitaji upweke bali shirika. Ilikuwa ni kazi ya watu wote kwa

> imani kuwa 'asiyezika hazikwi.' Bali yakale ndo yamepita.
>
> Jinja Maloni alichimba na kutoa mchanga bila ya kupumzika ila mara chache tu alipopachika sigara mdomoni… (uk.46-50).

Mtafiti wa kazi hii kwa kutumia nadharia ya saikolojia Changanuzi katika aya hii amemuhakiki Safari kwa kumuelewa kuwa anaonesha kuwa jamii kutokana na umasikini kazi ambazo zilikuwa zikifanywa kijamii sasa mambo yamebadilika kazi hizo ngumu zimekuwa ajira. Mtafiti wa kazi hii baada ya kupitia kwa kina amegundua kwamba changamoto ya umasikini ndiyo iliyopelekea Jinja Maloni kufanya kazi ya uchimbaji wa makaburi peke yake kwa tamaa ya kupata kipato huku akiambukia machofu. Msaanii amemtumia muhusika Jinja Maloni ili kuonesha usawiri wa mwanamme na changamoto zinazomkabili zinavyochangia kutokufaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao. Pia Changamoto hii ya ummasikini ndiyo iliyopelekea akina Tino kuingi katika vitendo viovu kama vile vitendo vya ujambazi.Tino alilazimika kuiba fedha benki ili aweze kuokoa maisha ya mwanawe Cheche aliyekuwa ameumia kiuno.

### 4.1.2 Changamoto ya Rushwa

Changamoto nyengine inayowakabili wanaumme katika kuchangia kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia ni rushwa (Chuachua na Wenzake, 2009; Taibu 2008; 2009; Mohd, 2012; Khatibu, 2014). Rushwa ni fedha au kitu cha thamani ambacho mtu hupewa au hupokea ili kununua au kuuza huduma ya kijamii ambayo haikustahiki kununuliwa kinyume na taratibu za utoaji wa huduma hiyo.Rushwa ni adui wa haki na maendeleo katika jamii yoyote. Mwandishi

wariwaya ya Joka la Mdimu Profesa Safari ameweza kubainisha tatizo la rushwa kama changamoto inayowakabili wanaume kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia. Mtafiti amegundua kwamba mwandishi wa riwaya hii ameweza pia kuizungumzia rushwa kama ni kichocheo cha hali mbaya ya maisha. Mtafiti ameiona hali hii ya rushwa ilivyoenea hadi katika sekta ya usafiri. Watu wanaingia katika gharama ambazo si za lazima. Katika kushadidia kuhusu rushwa na kuonesha kama changamoto inayowakabili wanaume kushindwa kupata maendeleo, mwandishi anamuonesha muhusika Amani namna anavyompa rushwa (mwenyewe anaiita ofa) dokta Mikwala ili amuandikie cheti cha kwenda Uengereza kwa matibabu. Mwandishi anasema:

> Mazungumzo machache yaliendelea mpaka pale Amani alipokusudia kulivunja baraza kwa kusema, Daktari nashukuru sana. Ngoja nikuache: Akachomoa kitita cha noti na kumkabidhi,…’ (uk.133*).*

Mtafiti amegundua kuwa, msanii amewatumia wahusika Amani na dokta Mikwala wote wakiwa wa jinsia moja ya kiume kama viashiria wa dhana hii ya rushwa. Amani akiwa mtoa rushwa na dokta Mikwala akiwa mpokeaji. Jambo hililinapelekea hali ya nchi kuzorota na kufanya watoto wenye matatizo mbalimbali kulazimika kutumia rasilimali zao ili kuhonga watumishi wa umma ili waewze kuwapatia huduma au upendeleo fulani kama ilivyojiri kwa Amani na dokta Mikwala. Kama sio rushwa rasilimali hizi zengeweza kutumika katika shughuli nyengine za kimaendeleo kama vil elimu, biashara, kilimo ambazo zingeweza kuondosha changamoto walizonazo wanaume zinazopelekea kutofaulu na kutopata maendeleo.

Kwa upande wa riwaya ya Joka la Mdimu pia kunajitokeza changamoto ya rushwa kama ifuatavyo :

> Lakini Brown Kwacha alikuwa mtu wa nyendo, akajua karata gani acheze na ipi abakishe. Alisema kwa kiburi, suala si kupata kiwanja ila mahali panapofaa kuporomosha kasri la fahari. Basi kwa muda wa juma, kila jioni aliendesha gari lake sehemu mbalimbali za ufukwe wa bahari kutafuta mahali pakumfaa.Hatimaye alipata sehemu mbili, ikawa aamue achague ipi.Bali uamuzi huo ulimuiya vigumu. Alirejea nyumbani kutafakari bila ya kumuhusisha mkewe. Zaidi ya miaka sita sasa alikuwa hamshirikishi mkewe katika maamuzi yake yoyote. Hakumtaka la heri wala shari. Baada ya kuwaza sana alipata wazo la kuvichukua viwanja vyote. Akajenga kimoja baada ya kingine. La'ta khofu, fedha si tatizo.
>
> Na kweli, juma lililofuata uamuzi wake huo alikwenda kuonana na Mkurugenzi wa Jiji. Mwenyekiti wa kamati ya kugawa viwanje aliitwa na kutakiwa aweke jina la Brown Kwacha katika orodha ya wanaopendekezwa kupatiwa viwanja. Basi, juma lililofuta Brown Kwacha akawasilishiwahati mbili za kumiliki viwanja, tena vile alivyovitaka.

Baada ya kupitia kwa kina maelezo haya ya msanii, mtafiti wa kazi hii amegundu kuwa, Brown Kwacha ametumia rushwa katika kuvipata viwanja hivi viwili tena kwa wakati aliotaka mwenyewe na viwanja vilevile alivyojichagulia mwenyewe, hukuakiwacha kundi la wengine wakipigwa danadana ama kweli usipokubali kuliwa huli waswhili walisema. Tukirejea tena kwenye maelezo haya utagundua kuwa wahusika wate aliowatumia mtunzi wa kazi hii; Profesa Safari utagundua ni wahusika wajinsia ya kiume. Kwa kutumia nadharia ya Mwiitiko wa Msomaji, mtafiti anaona rushwa ni changamoto nyengine inayawakabili wanaume kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao. Mtafiti ameona kuwa rushwa ndiyo

inayapelekea baadhi ya watu kuamua kujenga kwenye maporomoko na hata mitaro ya maji machafu.

### 4.1.3 Changamoto ya Ulevi

Changamoto nyengine inayowakabili wanaume kutofaulu kupata maendeleo katika jamii zao au taasisi wanazozisimamia ni ulevi. Mtafiti aligundu kuwa kuna ulevi wa aina mbili; Ulevi wa pombe na ulevi wa wanawake katika riwaya teule.

#### 4.1.3.1 Changamoto ya Ulevi wa Pombe

Kupitia muhusika Mzee Lomolomo Profsa Emmanuel Mbogo katika kitabu chake cha *Watoto wa Mama N'tilie* anasema:

> Mara nyingi Peter alikwishamsikia mama yake akimkataza baba yake kuimba wimbo wake huu. Utamsikia maman'tilie akigomba, '*Aa ! Bwana we ! Ndio nyimbo gani hizo,ee !'*
>
> Lakini Lomolomo hakumsikiliza, aliendelea kuimba. Mdomo wake uliokaa kama bakuli la pombe, ulitamka maneno kwa taabu. Kila alipoimba wimbo huu alichezesha mabega yake. Mabega yenyewe, tayari yalikuwa yamechonga kwa pombe ya gongo, yameangalia juuu karibu yakutane na masikio (uk.10-12).

Mtafiti wa kazi hii amebaini kuwa kwa kutumia muhusika Lomolomo, Mbogo anaisawiri barabara changamoto hii ya mapenzi ya ulevi hasa kwa wanaume waliokosa kazi au kusimamishwa kutoka makazini mwao. Hivi ndivyo ilivyo kwa jamii ya Kitanzania kwani wamo akina Lomolomo wengi. Hawa wanaendeleza pombe badala ya kufanya kazi. Changamoto hii inakuwa ni kikwazo ambacho huwafanya wanaume wengi kushindwa na kutofaulu kupata maendeleo ndani ya jamii zao na ndivyo ilivyokuwa kwa Mzee Lombolombo, ameshindwa kuwalipia

watoto wake ada za masomo shuleni na kupelekea watoto hao kufukuzwa shule na hatimae watoto hao kujiingiza kwenye vitendo viovu baada ya kushindikana kabisa kurudi shuleni na kuendelea na masomo.

#### 4.1.3.2 Changamoto ya Ulevi dhidi ya Wanawake

Changamoto nyengine inayowakabili wanaume ni mapenzi ya wanawake (Foiba, 2013). Mapenzi yasio ya kweli, mapenzi ya uongo yanayozingatia pesa tu.Mwandishi wa riwaya ya *Joko la Mdimu* Safari anatuanikia mapenzi ya uongo kupitia Muhusi kawake Brown Kwacha na wanawke zake kama vile Josphine, Laila na wengine wengi. Mapenzi ya wanawake hawa yaliegemea katika pesa na hayakuwa mapenzi yakweli. Mwandishi anaelezea:

BROWN KWACHA alitoa udhuru wa kutokuwepo kazini kwa siku tatu. Akaanza maandalizi ya safari yake ya kwenda Kwale. Safari hii ilikuwa kwa minajili miwili, mosi, kutimiza miadi ya kuonana na maashuki wake Laila. Pili, kwenda kuonana na wawindaji wake ilikupata vipusa alivyomuahidi Shirazi Bhanj (uk.108). Brown Kwacha alimlaki Leila kwa shauku kubwa, wakingia ndani ya ile Range Rover yake hadi Hotel ya Flamingo iliyokuwa maarufu kwa uzuri, huduma na ughali wake kupita zote mjini Kwale. Brown Kwacha alikuwa wa kwanza kuamka, uzingizi bado umemjaa machoni. Usiku uliopita fikra nyingi zilimduru akilini. Pale kitandani alimgeukia Leila ambaye bado alikuwa amelala fofofo. Safari za kila mara, usiku, mchana zilimnyima wasaa wa kulala vizuri. Nywele zake ndefu, masikio na pua ya upanga vilijitokeza nje ya shuka nyeupe na blanketi zito la rangi ya kijani nyepesi. Brown Kwacha alimtazama mno, moyo wake ukampapa, baada muda alishuka taratibu pale kitandani pajama. Aliingia bafuni, jirani tu na kitanda hicho, akafungua

kibomba ambacho kilichanganya maji ya moto na baridi, akanza kuoga taratibu.Aliporejea mle chumbani akamkuta Leila ameshamka bado kalala chali, safari hii kichwa kilikuwa kiko nje. Alimuangalia Brown Kwacha kwa makini, bila ya kusema kitu.

Hapa mtafiti wa kazi hii kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi amegundua changamoto inayowakumba wanaume wengi katika jamii yetu hii ya Kitanzania. Bronw Kwacha anaanga kazini kwa muda wa siku tatu na kutumia fedha za umma kwa ajili ya kumfuata mwanamke kwa lengo la kwenda kufanya mapenzi, mapenzi ambayo si yahalali.Hii ni changamoto inayokwamisha wanaume wengi wasiweze kufikia malengo ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia. Akina Brown Kwacha tunao wengi ndani ya jamii zetu. Msanii Safari amemtumia Brown Kwacha kama kielelezo tu kwa jamii husika.

### 4.1.4 Changamoto ya Kukosa Uaminifu

Changamoto nyengine ambayo inawakumba wanaume wengi na ambayo husababisha kutokufanikiwa kupata maendeleo ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia ni kukosa uaminifu (Chuachua, 2011 ; Ambrose, 2014). Safari kupitia riwaya yake ya *Joka la Mdimu* anatuonesha viongozi wakubwa wa serekali walivyokosa uaminifu kwanza kwa kutumia mali ya umma kuendesha maisha yao na kuwaacha raiya wao hasa wakulima wakiteseka na maisha hasa vijijini. Wakulima kwa upande wao vijijini nao wanakabiliwa na hii hali ngumu ya uchumi. Mazao ya biashara wanalima lakini hayawasaidii chochote kuinua hali zao za maisha, kwani wanaofaidi jasho la wakulima ni viongozi wachache. Matokeo ya yote hayo ni wakulima kuacha kulima mazao hayo ya biashara, msanii anasema:

> 'Ila kwa kifupi huko atokako watu wameacha kulima kahawa kabisa hawataki.'
> 'Kwa nini ?'
> 'Kipato kidogo, fedha yote yenda serikalini.Sijui tunaelewana ?'
> 'Naam ! Kutafuta fedha za kigeni kwa ajili yao hao wakubwa'
> 'Halafu hakuna anayeziona ! Kulima walime wao, kufaidi wafaidi wengine'
> 'Sasa wafanya nini ?'
> 'Wanalima nyanya.Fedha chapu chapu (Uk.39-40).'

Mwandishi hapa anatuonesha namna viongozi walivyokosa uaminifu. Wanachi (wakulima) wanalalamika kuwalalamikia viongozi kwa madai yao yakwamba wanatafuta fedha za kigeni lakini fedha hizo za kigeni zinaishia kwenye mikono ya wakubwa, jambo ambalo linawafanya wakulima waache kabisa kulima mazao ya biashara na kuamua kulima nyanya. Yote haya yanatokana na kukosa uaminifu.

## 4.2 Usawiri wa Mwanamme katika Riwaya Teule

Maanaya Usawiri ilishaelezwa katika sura ya pili ya utafiti huu.Katika kipengele hiki ambacho kinajibu swali la tatu la utafiti huu ambacho ni muhimu sana kwetu na ndio roho ya utafiti huu, kabla ya kuendelea mbele tutarudi tena kuonesha umuhimu wa kuchunguza usawiri wa muhusika mwanamme katkika dhamira za riwaya tulizozichagua *Joka La Mdimu* iliyoandikwa na Profesa Jumbe Safari na *Watoto wa Mama N'tilie* iliyoandikwa na Profesa Emmanuel Mbogo.

Mwanamme na mwanamke ni jinsia mbili muhimu sana katika kuijenga dhana ya Riwaya ili kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Waandishi wengi wa Riwaya huzitumia jinsia mbili hizi kama wahusika katika Riwaya zao. Mwanamme na mwanamke ni jinsia mbili ambazo katu mwandishi hawezi kuzitenganisha na bado

kazi yake ikabaki kuwa salama na yenye maana, nikama vile fani na maudhui niwatoto pacha. Bila ya fani huwezi kupata maudhui na bila ya maudhui huwe kupata Fani. Kwahivyo, mwandishi yeyote hawezi kuizungumzia fani tu bila ya kuwepo maudhui na kazi ikaweza kuleta manufaa kwa wasomaji. Nisawa na kuwepo kwa ardhi bila ya kiwepo kwa mbingu. Mbingu na ardhi kwapamoja ndizo zilizofanya Dunia leo ibaki kuitwa Dunia. Yote haya tunatilia mkazo kuwa kazi yoyote ya fasihi haiwezi kupendeza na hata kukamilika iwapo hakuihusisha na mwanamke na Mwanamme, na ndivyo wafanyavyo takribani waandishi wengi wa Riwaya  za Kiswahili na nyenginezo.

Siowengi ambao hupenda kuzungumzia nafasi ya mwanamme, jambo hili linaonekena ni geni sana kwenye masikio ya wasikilizaji, akili za wasomaji na hata macho ya watazamaji. Kwa kuwa wahakiki wengi na wachambuzi wengi na kwamara nyingi wamekuwa wakiitupia macho zaidi nafasi ya mwanamke tu, ilihali waandishi katika vitabu vyao huwa wanasawiri hali ya mwanamke na hali ya mwanamme pia, wote kwa pamoja waandishi huwa wanawachora kama sehemu ya jamii wanaowakilisha jamii husika. Hivyo, kubakia kumjadili mwanamke pekee bila ya kumtupia macho mwanamme na kumuangalia jinsi mwandishi alivyomchora, huenda tusifikie malengo na dhamira hasa alizokusudia mwandishi wa Riwaya husika.

Sasa, kwa kutumia nadhria ya Saikolojia Changanuzi ambayo msingi wake mkuu ni kuhusisha kazi ya fasihi na maisha ya mwandishi, historia au jamii yake (alichokiandika mwandishi kitakuwa kimemgusa mwandishi mwenyewe au jamii yake), nadharia ya Sosholojia ya Fasihi zimemsaidia mtafiti wa kazi hii  katika

kuchunguza usawiri wa mwanamme katika riwaya ya *Joka la Mdimu* iliyoandikwa na Profesa Safari na riwaya ya *Watoto wa Mama N'tilie* iliyoandikwa na Profesa Emmanuel Mbogo.

### 4.2.1 Usawiri wa Mwanamme kama mtu asiyeweza kufikiri bila ya Kilevi

Profesa Safari, katika kitabu chake cha *Joka La Mdimu* kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi anamsawiri mwanamme kama mtu asiyeweza kufikiria wala kuwaza chochote cha maana bila ya kupata uraibu (kilevi) kama vile sigara, mwandishi analithibitisha hilo kwa kupitia Muhusika Amini (uk-4) mwandishi anasema:

Saa mezani iliendelea kugonga taratibu, ta'ta'ta' ghafla ikaanza kutoa mlio mkali wa kengele. Amani, aliyekuwa akikoroma kitandani, si mbali na saa hiyo, alizinduka. Alijiinua sehemu ya kifua chake, halafu akalala tena. Sasa aligeuza uso wake tu kuangalia mishale ya ile saa ambayo ilionesha saa kumi na mbili asubuhi.Baadaye alipindukia upande wa pili kama kuisusia ile saa.Ghafla tena akageuka na kulala chali. Alibaki katika hali hiyo kwa kitambo akifikiri. Lakini hata fikira nazo zilikuwa kama zimempiga chenga, akapindukia tena upande ule wa saa na kuchukua paketi ya sigara juu yameza. Alichomoa sigara moja, akaipachika mdomoni, akaminya kibiriti cha gesi alichokichukua chini ya mto wake. Kwa muda, aliuangalia moto mwembamba wa buluu kabla ya kuubandika juu yancha ya sigara ile ndefu. Alikizima kile kibiriti na kuvuta mafunda mawili kwa mkupuo.Moshi wa sigara uliingi ndani ya mapafu ukaamsha vuguvugu na taratibu ulimalizasafari zake puani, kwa kutoka moshi katika mionzi ya pua. Naam, alichangamka kuliko awali. Alibaki amelala hivyo huku akitafakari mambo kwa wepesi na usahihi zaidi.

Hapa, mtafiti wa kazi hii, kwa kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi amegundua kuwa mwandishi anatuonesha fikra za Amani zimewea kutindimaa na kuchangamka baada ya kuvuta sigara. Hivi ndivyo aonavyo Profesa Safari katika kitabu chake cha *Joka la Mdimu*.

Pia mwandishi ameonesha hali kama hii katika (Uk-13) Mwandishi anasema:

Baada ya robo saa tu Amani alilipa fedha pale kaunta na kutoka nje. Jua lilikuwa limepanda na joto kuongezeka zaidi.Baada ya kuketi vizuri ndani ya gari, Amani alichukua paketi mpya ya sigara, akaichana vizuri, akaipigapiga juu kwa kidole chake, mara moja, mara mbili, na vichungi vya sigara mbili vikajitokeza na kupanda juu ya ganda la pakati hiyo. Alichomoa moja na kuiwasha. Alivuta mkupuo mmaja wapili na watatu. Barabara, alikuwa *na mazoea hayo kila baada ya kula ili* kuweka akili sawa.

Kwa kutumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi Profesa Safari anaona kuwa mawazo ya mwanamme hayawezi kutindimaa bila ya kupata uraibu kama vile sigara, mwandishi alimtumia muhusaka Aman kama kielelezo. Mtafiti wa kazi hii kupitia nadharia ya Sosholojia ya fasihi baada ya uchambuzi wa data za utafiti huu ameona akina Amani wako wengi mitaani ambao hawawezi kufikiri bila ya kilevi wenyewe wamezoeya kuuita uraibu. Hali kama hii pia imedhihiri kupitia muhusika Lomolomo katika riwaya ya Profesa Mbogo ndani ya kitabu chake cha *Watoto wa Mama N'tilie.*

### 4.2.2 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu asiye Muaminifu

Mwandishi wa *Joka La Mdimu* Kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi na nadharia ya Saikolojia Changanuzi Profesa Safari katika riwaya yake hii anamsawiri

mwanamme kama ni kijana asiye muaminifu kazini, mwenye tabia ya wizi (Uk-15) kwa kupitia muhusika Zitto mwandishi anatueleza:

Mwendo mfupi kuwasili Sega, alimuona kijana mrefu mpana akimpungia mkono kwa nguvu sana. Amani alibadili gea moja baada ya nyengine na kusimama mbali ya yule kijana. Upesi aliweka gea ya kurudi nyuma.Alimtambua yulekijana akasema, Vipi Zitto?

Nisevu unitupe poti maana nimeshachelewa. Wewe kila siku kuchelewa tu''. Amani alilalamika, 'Sasa nitakupeleka na nini nami petroli sina? Lakini Zitto alikuwa ameshaigia ndani na kuketi mbele. Twende tu bwana, ikizimika nitakuibia katika magari ya Bandari.'

Hapa mtafiti wa kazi hii kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi amegundua nidhamu ya wizi, jambo ambalo linaashiria kutokuwa na uaminifu tendo la kutaka kuiba mafuta hasa katika kampuni ambako muhusika anafanyia kazi ni wazi kwamba uadilifu umekosekana haikupaswa kwa muhusika Zitto kwa tamko lake alilomwambia Amani dereva wa teksi wewe twenda tu ikizimika nitakuibia katika magari ya Bandari hii ni kukosa uaminifu Zitto amegeuka kuku alalapo ndipo anyapo. Akina zito wako wengi ndivyo anavyotujuvya Profesa katika riwaya yake hii *Joka la Mdimu*. Hali kama hiyo ya kukosa uaminifu imejitokeza pia katika riwaya ya *Mama N'tilie* kupitia muhusika Musa, Peter na Dani (Uk.38) mwandishi anasema:

> ‘Alipoingia kituo cha basi hakutoka mikono mitupu.Wasafiri wanawake wengesikika wakilia machozi…’ Alipoingia dukani, Dani, bila mhindi kujua, alitoka na saa, *bangili, mkufu wa dhahabu ama chochote ambacho angekiuza, akapata pesa akala, akashiba.*’

Mtafiti amegundua kwamba muhusika Dani hakuwa muaminifu kitendo cha wizi kuibia wasafiri ndani ya vituo vya basi au katika maduka ya wahindi vyote hivi vinafahamisha kutokuwa na uadilifu na ndivyo walivyo wanaume wengi waishio mijini bila ya kazi yoyote.

### 4.2.3 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Muwelewa

Mwanamme amesawiriwa katika *Joka la Mdimu* kama ni mtu muelewa aliyechoshwa na hali mbaya ya nchi na visingizio visivyokuwa na msingi, lakini hana la kufanya ila nikusikitika tu. Mwandishi anatueleza katika (Uk.16):

> ‘Tumechoshwa na wimbo huo.Visingiwio tele.Hiki mara kile.Eti dunia nzima inamatatizo ya uchumi". "Sikweli.Tunazungumza na mabaharia kutoka nchi nyengine Afrika ambako hali si mbaya.Uongo mtupu tu." Hebu angalia hili tatizo lamafuta.Nasikia meli imekuja na mafuta, benki hatuna hata senti yafedha ya kigeni. Imegeuza na kurudi na kutuachia deni la kusafirisha mafuta hayo pamoja na ushuru wa bandari.Sasa kama usemavyo sukari inapelekwa nje, mbona tunashindwa kulipia mafuta?’

Katika maaelezo haya mtafiti amegundua kwamba kuna wanaume wasiodanganyika wanye uwelewa wa hali ya juu, juu ya mwenendo mzima wa hali halisi ilivyo duniani hawakubaliani kabisa na porojo za viongozi. Tafsiri ya uoni huu ni ya mtafiti aliyeihakiki saikolojia ya msanii kwa kutumia nadharia ya Saikolojia Changnuzi kwa mujibu wa Sigmund alivyosema kuwa mwanaadamu anakuwa na ung’amuzi bwete ambao huhodhi fikra na mitazamo hasi ambayo haiwezi kukubalika

na jamii. Hofu na mawazo hayo huweza kujitokeza katika hali tatu ambazo ni utani, ndoto, na uandishi.

### 4.2.4 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu mwenye Huruma

Profesa Safari katika kitabu chake hiki cha *Joka La Mdimu* (uk-26) kupitia muhusika wake Mkuu Amani anaona kuwa mwanamme ni mtu mwenye huruma asiyependa kufanya maovu. Mwandishi anasema:

> ‘Amani alijizuiya kufanya yote hayo hususan ukuwadi. Kwa hilo, nadhari yake ilimkatalia katakata.Nawakati alipowapakia wasichana wa kiafrika kuja kule kutafuta muradi wao aliingiwa na hofu za aina mbili.Kwanza, utu na usalama wa wasichana wale. Pili, hali ile ingeendelea hadi lini?’

Kutokana na maelezo haya, mwandishi anatudhihirishia jinsi mwanamme alivyo na huruma hasa kwa wanawake mtafiti amegundua usawiri wa mwanamme anavyomsikitikia mwanamke na kumuonea huruma. Katika maelezo yake muhusika Amani katika nukuu ya hapo juu jinsi anapoingiwa nahofu kwa wanawake wa kiafrika wanapokwenda kutafuta muradi wao na kujiuliza kwa hofu hali hii itaendelea hadi lini, kwa mawazo ya mtafiti maelezo haya yanampa tafsiri ya huruma. Hivyo kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji mtafiti anamuona mwanamme ni mtu mwenye huruma.

### 4.2.5 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Mpumbavu

Katika *Joka la Mdimu* Mwandishi anamuona mwanamme kuwa ni mtu mpumbavu, anayependa starehe, asiyejua ukweli kuhusu maisha. Anapambana na kazi ngumu na dhalili kama vile kuchimba vyoo na kuvitapisha, kulima nakadhalika. Mwandishi anasema:

> ‘Wa geto!’ Sauti yachini ya Jinja iliita kusalimu kama kawaida yake. Na bila kugeuka wala kuacha ‘kadhia’ yake wakati ule Tino aliitika, ‘sema Mzulu’.
>
> ‘Ni ndimi Gotagota, mwana wa Mfalme Chaka’, Jinja alijigamba kwa sauti nzito. Tino aligeuka kumuangalia mpangaji rafiki yake akitabasamu.

Jinja Maloni, kama mwenyewe alivyostahabu kuitwa, Mzulu, alikuwa na umri usiopungua miaka hamsini. Mrefu wa futu sita, mwili wake ulianza kuchoka kutokana na kazi nyingi za sulubu alizozipitia kama kuli na kadhalika.Hata hivyo alikuwa na mshipa mzuri na wahuni wa Sega walihara kumuingia. Alitembea kokote, wakati wowote bila ya kuhofia chochote.Zama za ujana wake alikuwa bondia na kupata zawadi kem kem kutoka kwa mabaharia wa meli za nchi mbalimbali. Katika kipindi hicho alifanya starehe za kila aina, akabadilisha wanawake kama mashati. Ila wakati haukumkopesha. Hatimaye Jinja alistaafu bila ya kudiriki mke wala mwana. Akaziponda pesa zake za kiinua mgongo kwa kunywa pombe za fahari hadi zilipokwisha. Hana kibanda hana kitanda. Ndipo akatokea Tino na kumpangisha katika kibanda chake. Jinja hakuchagua tena kibarua; akachimba vyoo, kuvitapisha, kulima na chochote ambacho mikono yake iliangukia mradi tonge kinywani (U k-32).

Katika nukuu hii mwandishi aliposema muhusika Jinja Maloni alistaafu kazi bila ya kuwa na mke wala watoto na fesa zote za kiinua mgongo akaziponda kwa kujwa pombe za fahari hadi zilipokwisha han ahana kibanda hana kitanda. Mtafiti wa kazi hii, kwa kurejelea nadharia ya Mwitiko wa Msomaji hapa amegundua kwamba alilolifanya Jinja ni upumbavu au tunaweza kuita uzembe. Badala ya kutumia kiinua chake mgongo vizuri badala yake anajiingiza kwenye anasa hatimaye anapangisha

kwenye kibanda cha rafiki yake Tino. Hali kama hii pia inajitokeza kwa muhusika Lomolomo katika riwaya ya Watoto wa Mama N'tilie. (Uk.10, 70, 71, 72). Mzee Lomolomo anaonekana mpumbavu kwa kuiwacha familia yake iteseke na badala yake yeye kujishughulisha na pombe. Mwandishi anatubainishia kwa kusema:

Tangu alipoachishwa kazi kule bandarini, Mzee Lomolomo amekuwa yeye na pombe na pombe na yeye. Hafanyi shughuli yoyote ya kumletea kipto bali akiamka asubuhi anakwenda kwenye vikao vya pombe, anarudi jioni au usiku akiwa nzwi (Uk. 13).

Kwa kumtumia mhusika Lomolomo, Emmanuel Mbogo anamsawiri barabara mwanamme hasa wa jamii ya Kitanzania kwani wamo akina Lomolomo wengi. Hivi ndivyo aonavyo mtafiti.

### 4.2.6 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu anayependa Ugomvi

Kwa kupitia muhusika Mkuu Tino Profesa Safari katika kitabu chake cha Joka La Mdimu anaona kuwa mwanamme ni mtu anayependa ugomvi.Anapenda kuona watu wanapigana na kuwakataza wale waliotaka kuwatenganisha ili wasiendelee na ugomvi huo (uk-35).

> 'Wacha kunisukuma, mshenzi wee!'
> 'Mshenzi mimi?'

Wavuta makwama wale wawili walijibizana kabla hawajavaana kupigania yale matenga. Watu walitaka kuwatenganisha lakini Tino aliwazuiya akashabikia, 'Wacheni wafanye mazoezi kidogo.' Lakini hayakuwa mazoezi bali malau. Huyu alitupa ngumi, mwengine alikwepa. Akarusha kichwa, teke, ngumi tena, hivo hivyo hadi pumzi zikawaishia.

Katika maelezo haya mwandishi anaonesha namna mwanamme anvyopenda ugomvi pale muhusika Tino alipowauiya watu wanaotaka kuwatenganisha wanogombana yeye Tino anasikika akisema “Wacheni wafanye mazoezi kidogo” kauli hii inaashiria kupenda ugomvi watu wanataka kuamuliwa yeye bado ameshikilia waachwe wafannye mazoezi. Mtafiti wa kazi hii anaona Tino kilichompelekea kutamka maneno hayo nikutokana na kuwa nimtu anayependa ugomvi.

### 4.2.7 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu aliyelaaniwa

Pia kupitia muhusika huyu Tino mwanamme anaonekana ni mtu aliyekumbana na laana zote za mjini, pombe, umalaya, wizi, ganja, ujambazi nakadhalika mfano (uk-39) Mwandishi anasema*: "Vipi, ulipata shida gani pale njiani?" Aliuliza yule mshitiri.*

> "Aaa! Limbukeni wa jiji wataka kunitia kash kash.Lakini hapa brek", Tino alijibu

Akaendelea, "Unasikia fadha, mimi hapa mjini nimemaliza. Nini ambacho sijafanya hapa mjini, labda"kugeuzwa". Mama vile! Lakini ganja nimevuta sana, gongo ndio kwao, kuiba nimeiba sana lakini nikashiti! "Wizi hauna maana!" alisisitiza tena huku akimtazama yule mshitiri wake ambae alijibu,"kweli bwana".

Laana ni matendo yote maovu ambayo ama Mungu Muumba ameyakataza au jamii husika. Hii ni tafisiri ya mtafiti. Msanii anapompamba muhusika wake kwasifa kama vile ulevi wa kuvuta bangi, gongo, wizi nakadhalika nikuonesha laana. Mtafiti wa kazi hii, baada ya kuyapitia kwa kina maelezo ya muhusika Tino wakati alipokuwa akimuhadisia mshitiri wake jinsi alivyoweza kufanya matendo ya laana ndipo mtafiti

wa kazi hii akaona kuwa msanii Profesa Safari kwa kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi amemsawiri mwanamme kama mtu walaana zote.

### 4.2.8 Usawiri wa Mwanamme kama *Mtu wa kufanya kazi Ngumu*

Profesa Safari anamuona mwanamme katika jamii yake ni mtu wa kufanya kazi ngumu kama vile uchimbaji wa kaburi, kupakua vyoo na kadhalika mfano mwandishi anasema:

“Baada ya mwendo mfupi, Jinja Maloni na wenzake waliingia katika eneo hilo huku yule mzee aliyekuwa kiongozi akisema taratiibu,"salaam alaikum mayitun", Jinja alishituka kusikia maiti wanasalimiwa, lakini yanini kuuliza kisa chake? Sururu na jembe begani, kurega mkononi, alipunguzahatua na kumuachia yule mzee aelekeze sehemu mahsusi ya kuchimba kaburi lenyewe la marehemu (Uk-45-46).

Suala la uchimbaji wa kaburi ni suala ambalo mara nyingi hufanywa kijamii, hasa kutokana na ugumu wa wake na namna linavyo tokezea, si suala la kujipangia. Hivyo, uchimbaji wa kaburi si kazi nyepesi.Mtafiti amegundua kwamba kupitia maelezo haya msanii anamsawiri mwanamme kama mtu wa kufanya kazi ngumu.

Pia katika (Uk-48 hadi 49) tunamuona Jinja Maloni akiwa katika shughuli za kupakua choo katika nyumba moja.Mwandishi anasema:

Siku iliyofuatia, Jinja Maloni alidamka kwenda kupakua choo katika nyumba moja. Alitia nguo zake za kazi ndani ya jumu lake pamoja na mafuta ya taa na kichupa kidogo cha manukato na sabuni kali ya marashi. Begani alipachika sururu na chepeo, mkononi kashika ndoo iliyofungwa kamba ndefu..

Mtafiti wa kazi hii baada ya kuzipitia data kwa kina mtafiti amegundua kuwa maelezo haya yanatuonesha wazi ugumu wa kazi yenyewe, kazi ya kupakua vyoo sio nyepesi, siwengi ambao wanaweza kuvumilia kuifanya. Msanii anamsawiri mwanamme akifanya kazi hii ya kupakua vyoo ili kudhihirisha kuwa mwanamme ni mtu wa kufanya kazi ngumu.

### 4.2.9 Usawiri wa Mwanamme kama Muombezi na Mtetezi wa Wanawake

Mwanamme pia anaonekana shujaa asiye ongopa katika kumtetea na kumnusuru mwanamke katika kundi la ubakaji (uk-52) Mwandishi anasema: “SAA tano na nusu usiku ule Jinja Maloni aliutipa mtindi wake ukamkubali. Alitembea na kupandisha kilima kurejea nyumbani kwake huku akiimba wimbo maarufu Mama yake na sofia. Lakini mwendo mfupi hafla, akakatishwa na sauti ya mkoromo kutoka kando kidogo ya barabara. Ilikuwa ni sauti ya mtu aliyefanya jitihada ya kuita msaada akashindwa.

Upesi Jinja alichomoa kurunzi yake kutoka mfuko wa nyuma wa suruali na kuiwasha. "Nafa! Niachieni shenzi...", sauti ya kike ilimfikia Jinja Maloni. Upesi alielekea pale kwa hadhari huku kakaza mikono.Alipapasa ala ya kisu alichokichomeka kiunoni ndani ya shati lake, akaridhika.

"Nani?" aliita. Hakukuwa na jibu. Wala hakuhitaji jibu kwani mwenye macho haambiwi tazama. Hatua chache kwenye nyasi chini ya kichakamwanamke mmoja alilazwa chali huku mwanamme amemkalia kichwani yumkini akimbana asipige kelele, mwanamume mwengine kapiga magoti miguuni, suruali kaishusha hadi magotini, jasho na udenda vikishindana.

"Mwacheni", Jinja alinguruma kama simba.

Lazima tumchangie kahaba huyu amekula nakunywa vyetu sana", lilikua jibu la yule aliyeshusha suruali magotini.

> "Uongo yule mwanamke alijitetea kwa shida.
> "Basi leo tutakuchapa alisema yule aliyemkalia mbele
> "Nasema, hamuwenzi", Jinja Maloni alikatisha, akimwiinua yule mwanamume..."

Mtafiti baada ya kuyasoma kwa kina maelezo haya amegundua kuwa muhusika Jinja Maloni ameonyesha ushujaa na msaada mkubwa kwa mwanamke ambaye tayari alikuwa ameshazibitiwa barabara na wabakaji tayari kwa kumfanyia vitendo viovu lakini Jinja Maloni kwa ujasiri kabisa akasema hamuwezi na kufanikiwa kumuinua mwanamke huyo. Hivyo kwa kutumia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi mtafiti anaona kuwa mwanamme ni muombezi na mtetezi wa wanawake.

### 4.2.10 Usawiri wa Mwanamme kama mtu Asiyechoka wala kuona Aibu

Mwanamme ni mtu wa kuhangaika katika kutafuta maisha, asiye choka, asiye ona aibu wala tabu, asiye na haya (uk-43). Kupitia muhusika Omar Mahafudhi, mwandishi anasema:

> "Omar Mahafudh, mfanya biashara maarufu, alikuwa mmojawa masalia ya Waarabu kutoka Omani. Zama hizo alizofika aliuza majora ya nguo, ambayo aliyabeba na kuzunguka nayo mitaani. Huku na huko alipita, vichochoroni, mabarabarani hadi majikoni akiwakopesha washitiri wake. Biashara haikuwa rahisi. Alitembea kwa mguu mwendo mrefu akipiga kelelekutangaza biashara yake kila baada ya mwendo mfupi, nguo!, nguo!, nguo!, Wengine walimkopa wakahama nyumba na madeni yao".

Kauli hii inatuwekea wazi kuwa mwanamme ni mtu asiyeona aibu wala kuchoka, kwani kutembea na majora ya vitambaa mitaani huku ukipiga kelele za mnada sio kazi rahisi, inahitaji jitihada na kutokuona aibu kama ambavyo msanii wa Joka La Mdimu alivyomsawiri muhusika wake huyu Omar Mahafudh kama ni kiwakilishi cha wanaume wengine walivyo.

#### 4.2.11Usawiri wa Mwanamme kama Mtu Mbakaji na Mnyanyasaji

Pia katika kipenge hiki, kwa upande mwengine mwandishi anamchora mwanamme kama mbakaji na mnyanyasaji wa wanawake kijinsia ni makatili wanaowatenza nguvu wanawake katika suala la mapenzi, kwa madai kuwa wameshawalilia vyao siku nyingi, suala ambalo linaonekana halina ukweli wowote isipokuwa nivishingizio tu vyakutaka kujengauhalali juu ya ubakaji wao huo (uk-53) mwandishi anasema:

> “Wewe unajua  tumepoteza gharama ngapi kwa fuska huyu!"?
> "Waongo, mahabithi wakubwa nyie. Hamna aibu! Mna fedha ya kuhonga nyie?
> "Yuke mwanamke alisema huku akizoazoa pale chini."

Kupitia maelezo haya mtafiti baada ya kupitia kwa kina data za utafiti huku akisaidiwa na nadharia ya Sosholojia ya Fasihi amebaini kuwa msanii wa riwaya ya *Joka la Mdimu* amemsawiri vilivyo mwanamme kama mtu mbakaji na mnyanyasaji wa wanawake.

#### 4.2.12 Mwanamme amesawiriwa kama Mtu Asiejiamini

Kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi Profesa Safari anamsawiri mwanamme kama mtu asiyejiamini, mshirikina mwandishi ameichora fikra ya mwanamme iamini kwamba pamoja na jitihada kubwa anayochukua, bodo mafanikio na ushindi hauwezi

kupatikana bila ya kwenda kwa mganga. Mwandishi anayadhihisha haya ndani ya kitabu chake cha *Joka la Mdimu* kupitia timu ya mpira ya Senga (Sega Warriors). Mwandishi anasema:

Mwisho kabisa, alibakia yule kiongozi na mzee mwingine mmoja wakizungumza taratibu kisha wakatoka hadi kwa mgangamaarufu kwa jina la Sangoma. Walipofika, walivua viatu mlangoni na kuingia ndani. Walikaribishwa na mtu mzima, kavaa fulana na kikoi.

"Ndio mmefuata ile shughuli yenu?"Akauliza.

"Naam! " Aliitikia yule kiongozi.Sangoma aliinuka na kwenda sehemu ya kando ya chumba chake kilichojaa vitabu na tunguri.Alichomoa kitabu kimoja kikukuu, akakipuulizia kama kufuta vumbi, alirejea kuketi pale chini kwenye msala kama walipo keti wale wageni wake. Alikifungua kile kitabu kwa makini.Alichukua miwani yake na kuipachika machoni juu ya pua.Ndipo alipoinua macho makavu kuwatazama wale viongozi wa Senga Warriors akasema bila tabasamu,"mchezo mgumu lakini msihofu.Shika hii!"Alitoa kitu kutoka kwenye koti na kumkabidhi yule kiongozi ambae alipokea kwa makini na hofu kiasi.Kisha wote wakatazamana kwa macho baridi mithili ya jogoo wanaotangaza vita.

"Nimekueza miiko yake", yule Sangoma alikumbusha..."

Mtafiti anaona suala la kwenda kwa mganga hasa katika maswala ya michezo ambayo yanahitaji utaalamu zaidi kuliko imani hasa zakishirikina ni kutojiamini. Pamoja na matayarisho yote waliyojitayarisha wachezaji wa timu ya Sega Warriors lakini bado viongozi wa timu hiyo hawajiamini wanaaona waende kwa babu.

### 4.2.13 Usawiri wa Mwanamme kama mtu Asiyejitambua

Safari anaona kuwa mwanamme ni mtu asiejitambua wakati anapopata ushindi au furaha, anaweza kutumia fedha zake nyingi sana bila ya kujali kwa vinywaji na starehe.Mwandishi anajaribu kuyaonesha hayo ndani ya kitabu chake cha *Joka la Mdimu* kupitia mhusika Amani (uk63) Mwandishi anaeleza:

“Amani alitia mkono mfukoni akachomoa kitita cha noti kunadi ufalme." Mpango upo. Chagueni mahali mpendapo. Pangoni, Ajax, Hilton, semeni! Gari lipo", aliwatazama sahibu zake dhahiri akifurahia mchezo safi waliocheza siku ile.

Mtafiti anaonakuwa kutumia fedha ovyoovyo kwa sababu ya ushindi nikutokujitambua, mwandishi wa riwaya hii ya *Joka la Mdimu* anamtumia muhusika Amani kama kielelezo tu kwa jamii. Mwandishi anaiambia jamii kupitia maneno haya ya Amani kuwa mwanamme ni mtu asiyejitambua hasa anapopata furaha au ushindi. Mtafit ametumia nadharia ya Saikolojia changanuzi ambapo muasisi wa nadharia hii anasema mwanaadamu anakuwa na ung’amuzi bwete ambao huhodhi fikra na mitazmo hasi ambayo haiwezi kukubalika na jamii. Hofu na mawazo hayo huweza kujitokeza katika hali tatu ambazo ni utani, ndoto na uandishi. Vilevile msanii wa riwaya ya Watoto wa Mama Ntilie kupitia nadhaia ya Saikolojia Changanuzi anamsawiri muhusika Lomolomo kama nimtu asiyejitambu kwa kuiwacha familia yake na badala yake anajihusisha na pombe (Uk. 13 ).

### 4.2.14 Mwanamme ni Mtu anayedanganyika Haraka

Mwandishi wa Joka La Mdimu kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi anamsawiri mwanamme kuwa ni mtu anayedanganyika haraka hasa katika suala la

mapenzi, kiasi ambacho kwa kumuona tu mwanamke kwa mara ya mwazo bila ya hata kufanya uchunguzi wa aina yoyote anaanza kuchanganyikiwa na damu kumuanza kutembea kwa kasi kwa tamaa za kimwili na mapenzi ya ovyo ovyo. Kwa kupitia muhusika Zitto mwandishi anasema:

Punde si punde alirejea na kuketi, kisha akafuatia msichana mmoja mnene, maji ya kunde, kajipiga khanga moja tu ya kijani iliyoandikwa: Kama umvuvi vua.Usicheze na Mashua. Alipopita Damu ya Zitto ilitembea kasi na mate yake kuwa mazito mithili ya jina lake. "Karibu", Zitto alishangiria ujaji ule huku akijisogeza pale alipokti kutoa nafasi kwa kimwana yule. Hali kama hiyo pia imdhihirishwa kwa muhusika Amani na muhusika Tino (UK-66).

Mtafiti amegundua kuwa mwanamme ni mtu anayedanganyika haraka hasa katika suala la kimapezi. Khanga aliyojipiga mwanammke aliyetokeza mbele ya Zitto ilitosha kumbabaisha na kumfanya achanganyikiwe nakupelekea kudanganyika kimapenzi. Pia kwa upende wa riwaya ya Watoto wa Mama Ntilie Profesa Mbogo naye kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi anamuonesha muhusika Peter akishawishiwa na Mussa ili aachane na Shule na badala yake ajiunge na biashara ya madawa ya kulevya, Peter anashawishika haraka bila ya kufikiri anajiunga na Musa (Uk.17-18 ).

### 4.2.15 Mwanamme ni Mtu mwenye Mapenzi Makubwa kwa Watoto wake

Kupitia kitabu hiki *Joka La Mdimu*, Profesa Safari kupitia nadharia ya Sosholojia ya Fasihi na nadharia ya Saikolojia Changanuzi anamsawiri mwanamme kuwa ni mtu

mwenye mapenzi makubwa sana kwa watoto wake hasa watoto wake wa kiume. Kwa kupitia muhusika Tino mwandishi anasimulia:

> “LILIPOBAKI juma moja kabla ya sikukuu ya Idd el Fitri, Tino alimchukua mkewe na watoto wao kwenda kutafuta nguo za iddi. Asubuhi moja yeye na mkewe tu, alichukuliwa na Amani hadi katika mtaa wa Uhuru katikati ya jiji la Mindul.Huko waliingia na kutoka duka hadi duka.Yote yalijazwa nguo, viatu, marashi na libasi nyngine nyingi za kuvutia mno.Bali mali ya macho haifungi mtumba. Kilichogomba bei. Wngenunua nguo ngapi. Mwisho waliamua kutia macho nuru tu.Upesi upesi waliyapitia maduka yote yasifa katika mtaa wa Uhuru kisha wakapanda basi kureja Sega. Siku iliyofuata walitoka na watoto hadi kwa Bobix Makaoni kutafuta vitu walivyoshindwa kuvinunua jana jijini Mandul.Saa nn4 asubuhi, lakini watu watu walikua kama utitiri. Hwa ilichafuka kwa wingi wa nyayo na tosi za wanamji huo”.

Mtafiti wa kazi hii, anaona tendo la kumchukua mtoto na mke kwenda nao madukani kwaajili ya kutafuta nguo hasa za siku kuu kunaonesha upendo wa hali ya juu kabisa. Mwandishi amemtumia muhusika Tino na watoto wake ili kuonesha namna mwanamme alivyo na mapenzi makubwa kwa kwa mke na watoto wake.

Pia kwa kupitia muhusika huyu huyu mwandishi anaonesha jinsi mwanamme alivyona mapnzi na watoto wake, pale Tino alipopata taarifa ya mtoto wake ya kulazwa Hospitali kwa njia ya telgramu ambayo ilikuwa imendikwa,"TINO SLP 1010, SEGA CHECHE KALAZWA HOSPITALI NJOO HARAKA MWEMA". Ilikuwa imandikwa na mkewe kutoka kijijini kwao.

Pamoja na shida kubwa iliyokuwepo ya usafiri Tino bila ya kujali alijutupa barabarani kwa kudandia magari ya mizigo na wakati mwngine akijikuta akitemba

kwa miguu bila woga ili kuwahi kwnda kuiona hali ya mtoto wake Cheche aliyekuwa amelazwa huko Midule (UK80-89).

### 4.2.16 Usawiri wa Mwanamme kama Mtu asiyependa Familia yake

Mwandishi wa riwaya ya *Joka la Mdimu* Profesa Jumbe Safari kupitia nadharia ya Saikolojia Changanuzi amemsawiri mwanamme kama mtu asiyeipenda familia yake.Kwa kupitia muhusika wake Mkuu Brow Kwacha na mke wake. Mwandishi anatuambia kwamba Brown Kwacha hakumpenda mke wake ndio maana alibadilisha wanawake kama nguo na bila kumjali mke wake. Nyumbani hakuwa na raha na mke wala watoto wake, kila siku visingizio (Uk.91). Kutokana na kutokuwa na uaminifu katika ndoa yake alifika hatua akawa anawaleta wanawake wanje hata nyumbani kwake kama anavyosema msanii:

> "Mke wake Kwacha aliwafumania nyumbani kwake wamejibwaga kitandani kalamu ikiandika" (Uk.94).

Tendo la mume kufikia hatua ya kuleta wanawake wanje ndani linaonesha wazi kutokuwepo kwa upendo ndani ya familia, kama ambavyo amefanya Brown Kwacha. Mtafiti wa kazi hii baada ya kupitia kwa kina data alizokusanya katika utafi huu na kuzichambua kwa kusaidiwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ameona kwamba hiyo ndiyo taswira ya wanaume wengi kukosa mapenzi kwa familia zao na badala yake kujiingiza katika dharau na mapenzi ya nje.

Mtafiti pia amegundua kuwa kukosa uaminifu na kutokuipenda familia huwa ndio chanzo cha mateso ndani ya nyumba na kukosekana kwa Amani ndani ya familia, mwandishi anasema:

> “Baina yake na mumewe palikuwa na mkato mithili ya wembe: Vigumu kuonekana kwa macho ila kwa madhara yake. Alikonda akajipa moyo, akarudisha hali yake, akakonda tena na tena” (Uk.104).

Kwa ujumla mtafiti wa kazi hii amegundua kuwa, kukosa uaminifu na upendo katika familia huwa ndio chanzo cha kuvuruga Amani na utulivu kati ya mke namume na watoto na matokeo yake ni kusambaratika kwa familia hiyo.

Kwa upande wa riwaya ya *Watoto wa Mama N’tilie* Profesa Emmanuel Mbongo naye anamsawiri mwanamme katika hali hiyohiyo ya kutopenda familia yake,kupitia muhusika Lomolomo mume wa Mama n’tilie Lomolomo nashinda kwenye ulevi wa changaa , mataputapu na gongo anaicha familia ikiteseka watoto wanafukuzwa Shule kwa kukosa ada na sare. Mama ntilie ndiye anayehangaika na watoto.Mtafiti baada ya uchambuzi wa data kupitia nadharia ya Mwitiko wa Msomaji amegundua kuwa Profesa Emmanuel Mbogo Kupitia Mzee Lomolomo anaisawiri barabara jamii ya wanaumme wa Kitanzania kwani wamo akina Lomolomo wengi.Hawa wanaendeleza pombe badala ya kushughulikia familia zao kwa kufanya kazi za kuwapati kipato cha halali na kuweza kuendeleza familia zao.

## 4.3 Hitimishi

Sura hii imejikita zaidi na uchambuzi wa data zautafiti zilizokusanywa na mtafiti wa kazi hii. Uchambuzi huu ulifanywa kwa mujibu wa malengo mahususi yaliyobainishwa ktika utafiti huu. Kila lengo moja liliweza kuchambuliwa kwa kuangalia data za utafiti zilizokusanywa maktabani na mtafiti wa kazi hii, ambazo ni kuchunguza usawiri wa Mwanamme kupitia riwaya mbili teule riwaya ya *Joka La Mdimu* ilyoandikwa na Profesa Abdalla Jumbe Safarina riwaya ya *Watoto wa Mama*

*N'tilie* iliyoandikwa na Profesa Emmanuel Mbogo.Mtafiti wa kazi hii aliongozwa na nadharia ya Saikolojia Changanuzi na nadharia ya Sosholojia ambazo ndizo zilizowezesha kukamilisha kazi ya uchambuzi.

# SURA YA TANO

# MUHUTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura hii ni ya mwisho ambayo inatoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. Sura hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni; sehemu ya kwanza inahusu muhtasari, sehemu ya pili inahusu hitimisho la utafiti huu na sehemu ya tatu ni mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.1 Muhutasari

Mtafiti alihusisha kitabu cha *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*ili kupata data za utafiti. Utafiti ulikuwa na jumla ya sura tano. Katika sura ya kwanza kuna utangulizi, katika utangulizi huo, mtafiti amebainisha mada ya utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti na maswali ya utafiti Pia, sehemu hiyo, imeonesha vikwazo vya utafiti na njia za utatuzi wa vikwazo hivo.

Katika sura ya pili, mtafiti ameonesha kazi kadhaa alizozitalii zinazohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti aligundua kuna nafasi ya kufanya utafiti huu, kwani mada hii haijafanyiwa utafiti wa kina. Vile vile katika sura hii mumeelezwa nadharia ya Sosholojia ya Fasihi na nadharia ya Saikolojia Changanuzi ambazo zilimuongoza mtafiti katika utafiti huu. Sura ya tatu ya utafiti huu imeelezea mbinu zilizotumika kukusanyia data na kuzichambua. Imeelezwa kuwa, utafiti huu niwamaktabani ambapo data zimekusanywa kutoka katika vitabu teule vya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Aidha, dataziliwasilishwa kwa njia ya usomaji makini na kuchambuliwa kwa njia ya kimaelezo. Pia, sura ya nne, imeshughulikia

uchambuzi na uwasilishaji wa data zilizokusanywa na mtafiti. Na sura ya tano inaelezea matokeo ya utafiti huu. Sura hii, imeelezea tathmini ya utafiti huu na mapendekezo ya utafiti. Mtafiti amegundua kuwa riwaya teule zimeonesha usawiri wa mwanamme kwa mawanda mapana kama malighafi ya kuzifanikisha riwaya hizo za Kiswahili. Matokeo hayo ya utafiti, kwamuhtasari, ni kama ifuatavyo:

### 5.1.1 Dhumuni Mahususi la Kwanza

Dhumuni la kwanza la utafiti lilikuwa kuchunguza Changamoto zilizojitokeza ndani ya riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Dhumuni hili liliongozwa na swali lisemalo "Ni changamoto zipi zinazochangi kutokufaulu kwa wanaume ndani ya jamii zao au taasisi wanazozisimamia zinazojitokeza ndani ya riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa mama N'tilie*?"

Katika utafiti huu, mtafiti aligundua kuwa, ndani ya kazi teule kumejitokeza Changamoto nyingi kama vile umasikini, rushwa, ulevi, wizi nakadhalika. Kwa ujumla vipengele hivyo ndivyo vilivyobeba ujumbe wa mwandishi. Kwa hali hiyo, mtafiti amebaini kwamba, kazi nyingi za fasihi ambayo imeandikwa haziwezi kuepuka vipengele vya changamoto hizi ingiwa si watafiti wengi ambao wanavishughulikia katika usanii wao.

### 5.1.2 Dhumuni Mahususi la Pili

Dhumuni la pili la utafiti lilihusu kuelezea usawiri wa mwanamme kama alivyosawiriwa ndani ya Riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa mama N'tilie.* Dhumuni hili liliongozwa na swali lisemalo: "kueleza usawiri wa mwanamme

katika riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie"*. Baada ya kuchambua data, mtafiti amegundua kwamba, kuna taswira mbali mbali zilizojitokeza katika riwaya ya *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Katika riwaya ya *Joka la Mdimu*, Mwanamme amesawiriwa kama: Kiumbe shujaa, Mtetezi na mkombozi wa wanawake, mpenda starehe, mnyonge anayestahiki kazi ngumu, mwenye huruma kwa mke na watoto, mtu asiyejali familia yake kutaja kwa uchache.

## 5.2 Hitimishi

Utafiti huu ulidhamiria kutafiti Usawiri wa mwanamme katika dhamira za riwaya mbili *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Utafiti ulikuwa wa maktabani. Pia uliongozwa na malengo mahususi matatu.Malengo hayo yalikuwa ni kubaini Changamoto zinazomkabili mwanamme kutokufaulu katika jamii zao au taasisi wanazozisimamia na Lengo mahususi la pili lilikuwa ni kubaini usawiri wa mwanamme katika riwaya mbili teule *Joka la Mdimu* na *Watoto wa Mama N'tilie*. Kwa jumla, tumeona kuwa mwanamme naye na anaweza kusawiriwa katika hali chanya na hasi kama ilivyo kwa mwanamke. Tumezoea kuona mwanamke akisawiriwa katika hali hasi kwa kiasi kikubwa na mwanamme akionekana kuwa yeye ni mtu mkamilifu asiyekuwa na matatizo yoyote lakini ukweli ni kwamba wote mwanamke na mwanamme kila mmoja ana mazuri na mabaya yake.

## 5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Mtafiti wa kazi hii anaamini kwamba, ameweza kutoa mchango mkubwa sana kupitia utafiti huu unaohusu kuchunguza Usawiri wa mwanamme katika dhamira za riwaya ya *Joka la Mdimu* iliyoandikwa na Profesa Jumbe Safari na riwaya ya *Watoto*

*wa Mama N'tilie* iliyoandikwa na Profesa Emmanuel Mbogo. Hata hivyo, mtafiti kwa upande mwengine kuwa hakuna utafiti unaoweza kukamilisha kila jambo.Kutokana na hali hiyo mtafiti anatoa mapendekezo yafuatayo:

### 5.3.1 Mapendekezo ya Kitaaluma

Wanataaluma sasa wajitupe katika kumchunguza na kumuangalia muhusika mwanamme, nimuhimu sana kwani waandishi/wasanii wanamsawiri muhusika huyu wa kiume kama kiwakilishi cha jamii husika. Si vyema kuendelea kuchunguza usawiri wa mwanamke ta jambo ambolo linapelekea kuiweke pembeni jamii kubwa na muhimu yanayowasibu wanawake yanawasibu pia wanaume japo kama wapo katika mfumo dume.

### 5.3.2 Mapendekezo ya Kijamii

Wanashauriwa wanajamii hasa wasomi wa riwaya waone jinsi wanaume wanavyo nyanyasika na kukosa haki zao za msingi pamoja na kujiingiza katika vitendo viovu, ili wasidharau kundi hili kubwa la wanaumme linalopotea huku ikidhaniwa kuwa ni wanawake tu ndio wanaonyaswa kuonewa na kudhulumiwa wanaume pia wananyanyasika nakuonewa.

### 5.3.3 Mapendekezo kwa Watafiti wa Usoni

Watafiti wengine wajitokeze kufanya tafiti za kitaaluma za wasanii hawa nawengine ili kufichuwa usawiri wa mwanamme ili kuendeleza hapa ambapo mtafiti wa kazi hii amefikia na kutoa mwanga Zaidi juu ya usawiri wa mwanamme katika riwaya au fasihi nyenginezo.

## MAREJELEO

Ali, S. (2013). "Athari za Mtindo katika Kuibua Maudhui: Mifano kutoka Bembezi Pemba." Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ambrose, B. M. (2014**). "**Kuchunguza Dhamira za Kisiasa katika Riwaya za Shaaban Robert Mfano wa Kusadikika na Kufikirika." Tasinifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania.

Ameir, I. H. (1983). *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. Dar es Salaam: TUKI.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research.* Belmont: Wadsworth Publishing Company.

Balisidia, M. L., (1987) "Tanzu na Fani za Fasihi Simulizi." *Katika Mulika* 19, Chuo Kikuu cha Dar-es-salaam: TUKI.

Bryman, A. (2004). *Social Research Methods*. Oxford: Oxford University.

Caleb, C. H. (2013). "Taswira ya Mwanamke katika Tamthilia ya Nguzo Mama na Mamae." Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi

Chuachua na Wenzake (2009). "Shaaban Robert: Visa na Ukoloni." Katika Mulika. Dar es Salaam: TUKI.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert*. Dar-es-salaam: TUKI.

Foiba, N. (2013). “Taswira ya Kifo cha Shujaa Katika Utendi.” Tasnifu ndogo ya Shahada ya Kwanza, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Furlong, N. (2000). *Research Methods and Statistics*: *An Intregrated Approach*, New York: Hartcourt Colledge Publishers.

Kenguru, P. J. M. (2013). “Fasihi Simulizi katika kazi ya Utu Bora Mkulima,” Tasinifu ya Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Khatib, M. S. (2014). *Chanjo*, *Matakwa ya Mwanamme katika Mwili wa Mwanamke*.” Dar es Salaam: TATAKI.

Kihore, Y. M. (1996). *Kozi ya Maandalizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kitula, M. (2010). “Research Methodology for Postgraduate Students.” The Open University of Tanzania.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis Writing: Introduction*. Nairobi: Paulines Publication Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods: Methods and Techniques*. New Delhi: Wiley Eastern Ltd.

Kothari, R. C. (2004). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Limited, Publishers.

Lyatuu, J. (2011). “Usawiri wa Mwanamke katika fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Mwandishi wa Kike na wa Kiume: Uchunguzi katika Riwaya Teule.” Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Kikuu cha Dar es Salaam.

Matteru, M. L. (1976). “Fani ya Hadithi na Riwaya: Makala katika Kioo cha Lugha.” Chuo Kikuu Cha Dar-es-salaam.

Mukobwa, M. (1985), “Maendeleo ya Kimaudhui katika Tamthiliya Tano za Hussein,” Tasinifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Mohd, S. (2012). “Uhalisia Mazingaombwe katika hadithi simulizi za FasihiSimulizi. Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Msokilie, B. (1993). *Miongozo ya Lugha na Fasihi: Uchambuzi na Uhakiki wa Riwaya*. Dar es Salaam: DUP.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi: Katika Mulika 21*. Dar es Salaam: TUKI.

Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mulokozi M. M. (2002). *Tenzi Tatu za Kale*. Dar-es Salaam: TUKI.

Mung’eri, O. B. (2000). “Utetezi wa Maandishi katika Fasihi: Nadhariya ya Shaaban Robert.” Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu Nairobi.

Ndungo C. M na Wafula R. M (1993). *Nadharia ya Fasihi Simulizi (Kiswahili part III).* Nairobi: Nairobi University Press.

Ndungo, W. C. na Mwai, R. (1991). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Nairobi University Press.

Njogu, K. na Rocha, C. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*: Nairobi, JKF.

Nkwera, F. M. V (1979). *Sarufi na Fasihi*: *Sekondari na Vyuo*. Dae-es- salaam: Tanzania Publishing House.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi.* Augustana College: Rock Island.

Nguta, C. (2011). "Fani na Usawiri wa Wahusika wa kike katika tamthilia ya *Pango* na *Mama ee*." Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ramadhan, S. (2013). "Usawiri wa Mwanamke katika Taarab ya Mipasho: Mfano kutoka nyimboza Mzee Yussuf Mzee." Shahada ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo T.S.Y na Kiango S. D. (1977). *Hisi Zetu.* TUKI: Dar-es salaam, Tanzania.

Sengo, T. S. Y. (1975). *Shaaban Robert*: *Uhakiki na Maandishi* Yake. Nairobi: Foundation Books.

Senkoro, F. V. (1976). *Utamaduni katika Riwaya za Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F. V. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press Publicity Centre.

Taib, A. H. (2008). "Mkabala wa Kiislamu katika Uchanganuzi na Uhakiki wa Fasihi ya Kiswahili." Makala katika Kongamano la CHAKAMA.

Taib, A. H. (2009). "Maisha ya Shaaban Robert na Falsafa yake katika Maandishi." *Katika Mulika.* TUKI: Dar-es-salaam.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Phonex Publisher Limited: Nairobi, Kenya.